

SHERIA YA MABADILIKO YA KATIBA

YALIYOMO

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Kanuni	Kichwa cha Habari	Ukurasa
1.	Jina	1
2.	Matumizi	1
3.	Tafsiri	1

SEHEMU YA PILI

HAKI, KINGA NA MADARAKA YA BUNGE MAALUM

4.	Bunge Maalum	3
5.	Mamlaka ya Bunge Maalum	3
6.	Haki na Kinga za Bunge Maalum	4
7.	Ukomo wa mamlaka ya Bunge Maalum	4

SEHEMU YA TATU

MIKUTANO NA VIKAO VYA BUNGE MAALUM

8.	Utaratibu wa ukaaji ndani ya Ukumbi wa Mikutano ya BungeMaalum	4
9.	Mkutano wa kwanza wa Bunge Maalum.....	5
10.	Shughuli za Mkutano wa Kwanza wa Bunge Maalum.....	5
11.	Utaratibu wa kumchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti	6
12.	Kiapo cha Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti.....	6
13.	Wimbo wa Taifa.....	7
14.	Dua ya kuiombea Jamhuri ya Muungano na Bunge Maalum.....	7
15.	Kiapo cha Mjumbe wa Bunge Maalum.....	7
16.	Mikutano ya Kawaida ya Bunge Maalum.....	8
17.	Utaratibu wa vikao vya Bunge Maalum.....	8
18.	Kuahirisha Mkutano wa Bunge Maalum.....	9
19.	Wajibu wa Mjumbe kuhudhuria Mikutano na vikao vya Bunge Maalum...	9

SEHEMU YA NNE

UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA BUNGE MAALUM

(a) Viongozi wa Bunge Maalum

20.	Mwenyekiti na mamlaka yake.....	10
21.	Makamu Mwenyekiti na majukumu	11
22.	Uadilifu kwa viongozi wa Bunge Maalum.....	12
23.	Katibu na Naibu Katibu wa Bunge Maalum.....	12
24.	Kazi na majukumu ya Katibu wa Bunge Maalum.....	12
25.	Naibu Katibu na majukumu yake.....	13

(b) Sekretarieti ya Bunge Maalum

26. Sekretarieti ya Bunge Maalum.....	13
---------------------------------------	----

(b) Uendeshaji wa Shughuli

27. Mpambe wa Bunge Maalum na majukumu yake.....	14
28. Upangaji wa muda wa kutekeleza shughuli.....	14

(d) Mpangilio wa Shughuli

29. Mpangilio wa Shughuli za Bunge Maalum	14
30. Taarifa ya Mwenyekiti.....	15
31. Mambo yanayohusu haki za Bunge Maalum	15

(e) Uhalali wa Shughuli

32. Akidi ya vikao vya Bunge Maalum	15
	16

(f) Utaratibu wa Kujadili Hoja

33. Utaratibu wa kujadili hoja.....	16
34. Kubadilisha hoja.....	16
35. Mabadiliko ya hoja na kuondoa hoja ya mabadiliko	17

SEHEMU YA TANO **KANUNI ZA MAJADILIANO**

36. Nyakati za Mjumbe kusema Bungeni	17
37. Jinsi ya kupata nafasi ya kusema Bungeni.....	18
38. Mambo yasiyoruhusiwa Bungeni.....	19
39. Muda wa kusema Bungeni.....	21
40. Kusema zaidi ya mara moja	21
41. Staha ndani ya Bunge	21
42. Mamlaka ya Mwenyekiti kukatiza majadiliano	22
43. Taarifa kuhusu utaratibu na Mwongozo wa Mwenyekiti	22
44. Hoja ya kuahirisha au kusitisha mjadala	23
45. Hoja ya kufunga mjadala	24
46. Hoja ya kufunga mjadala	24
47. Vikao vya faragha vya Bunge Maalum.....	25

SEHEMU YA SITA **KAMATI ZA BUNGE MAALUM**

48. Kamati za Bunge Maalum	25
----------------------------------	----

49. Muundo wa Kamati za Bunge Maalum	27
50. Utaratibu wa mikutano na vikao na akidi katika Kamati za Bunge	28
51. Vikao vya faragha vya Kamati za Bunge.	30
52. Majukumu ya Kamati ya shughuli za Bunge Maalum.....	30
53. Majukumu ya Kamati ya Kanuni na Haki za Bunge	30
54. Majukumu ya Kamati ya Uandishi	31
55. Majukumu ya Kamati Namba Moja.....	31
56. Majukumu ya Kamati Namba Mbili	31
57. Majukumu ya Kamati Namba Tatu	31
58. Majukumu ya Kamati Namba Nne.....	31
59. Majukumu ya Kamati Namba Tano.....	32
60. Majukumu ya Kamati Namba Sita.....	32
61. Majukumu ya Kamati Namba Saba	32
62. Majukumu ya Kamati Namba Nane	32
63. Majukumu ya Kamati Namba Tisa.....	33
64. Majukumu ya Kamati Namba Kumi.....	33
65. Majukumu ya Kamati Namba Kumi na Moja.....	33
66. Majukumu ya Kamati Namba Kumi na Mbili.....	33
67. Majukumu ya Kamati Namba Kumi na Tatu.....	34
68. Majukumu ya Kamati Namba Kumi na Nne.....	34
69. Majukumu ya Kamati Namba Kumi na Tano.....	34
70. Majukumu ya Kamati Namba Kumi na Sita.....	34
71. Majukumu ya Kamati Namba Kumi na Saba.....	35
72. Upangaji wa ratiba ya utekelezaji wa kazi na majukumu ya Bunge Maalum.....	35
73. Kazi za Kamati na Utekelezaji wake.....	35
74. Utaratibu wa Kufanya Maamuzi katika Kamati za Bunge.....	36
75. Wajibu wa Mjumbe kuhudhuria vikao na ukomo wa Kamati	36

SEHEMU YA SABA

UTARATIBU WA KUWASILISHA, KUJADILI NA KUPITISHA MASHARTI YA RASIMU YA KATIBA

76. Utaratibu wa Kuwasilisha Rasimu ya Katiba	37
77. Rasimu ya Katiba kupelekwa kwenye Kamati.....	37
78. Uwasilishaji wa Hoja ya Kamati	38
79. Masharti kuhusu mapendekezo ya marekebisho	39
80. Utaratibu wa majadiliano wakati wa kujadili taarifa ya Kamati.....	39
81. Utaratibu wa kupiga kura kupitisha mapendekezo ya marekebisho	40
82. Utaratibu wa kufanya uamuzi.....	41
83. Kura ya siri	41
84. Kura ya kielektroniki.....	42
85. Utaratibu wa kupiga kura na kupitisha masharti ya Rasimu ya Katiba	42
86. Utaratibu wa kupitisha Rasimu ya Katiba.....	43
87. Hoja ya kuwasilisha Rasimu ya Katiba.....	43
88. Kufanya masahihisho ya kuondoa makosa ya uchapishaji katika Rasimu ya Katiba.....	44
89. Ridhaa ya Bunge Maalum na hifadhi ya Rasimu ya Katiba.....	44

SEHEMU YA NANE
UTARATIBU WA KUTUNGA MASHARTI YA MPITO NA MASHARTI
YATOKANAYO

90. Utaratibu wa kutunga masharti ya mpito na masharti yatokanayo.....	44
--	----

SEHEMU YA TISA
AMANI NA UTULIVU BUNGENI

91. Mamlaka ya Mwenyekiti wa Bunge Maalum kusimamia utaratibu.....	45
92. Adhabu zinazoweza kutolewa na Mwenyekiti kwa ukiukwaji wa Kanuni	45
93. Adhabu zinazoweza kutolewa na Bunge kwa ukiukaji wa Kanuni.....	46
94. Mamlaka ya Mwenyekiti ya kuhakikisha amani na utulivu Bungeni	46
95. Masharti kwa Mjumbe aliyesimamishwa kazi	47
96. Mamlaka ya msamaha ya Mwenyekiti.....	47
97. Udhibiti wa fujo Bungeni	47
98. Wajibu wa Mjumbe kutunga amani na utulivu Bungeni.....	47

SEHEMU YA KUMI
WAGENI

99. Ruhusa ya wageni Bungeni.....	47
100. Ruhusa kwa Waandishi wa Habari	48
101. Mamlaka ya kuwaondoa wageni Bungeni.....	49

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
USALAMA WA MAENEO YA BUNGE MAALUM

102. Utaratibu wa kuingia maeneo ya Bunge	49
103. Ukaguzi	49

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
MENGINEYO

104. Lugha rasmi Bungeni	50
105. Stahili za Wajumbe na Watumishi wa Bunge Maalum	50
106. Taarifa Rasmi za Bunge.....	50
107. Mavazi Rasmi	51
108. Ufafanuzi kutoka Tume ya Mabadiliko ya Katiba	51
109. Utaratibu baada ya kifo ya Mjumbe	52
110. Maoni na ushauri wa kisheria kuhusu Kanuni za uendeshaji wa shughuli za Bunge Maalum	52
111. Kutengua Kanuni	51
112. Matumizi ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum	52
113. Kufanya mabadiliko au marekebisho katika Kanuni	52

NYONGEZA
KANUNI ZA UCHAGUZI WA MWENYEKITI NA MAKAMU MWENYEKITI

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

1.	Jina	53
2.	Matumizi	53
3.	Tafsiri	53

SEHEMU YA PILI
USIMAMIZI NA UCHAGUZI

4.	Uendeshaji na usimamizi wa uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum	54
5.	Kuwasilisha jina la mgombea	54

SEHEMU YA TATU
UPIGAJI WA KURA

6.	Kujitoa katika uchaguzi.....	54
7.	Upigaji wa kura	55

SEHEMU YA NNE
KUTANGAZA MATOKEO YA UCHAGUZI

8.	Kutangaza matokeo ya kura	55
9.	Mwenyekiti/Makamu Mwenyekiti kula yamini/viapo.....	56

FOMU YA KUPENDEKEZA JINA LA MGOMBEA
[Chini ya Kanuni ya 52(2)]

KUPENDEKEZA JINA LA MGOMBEA

A:	Wajumbe Kumi kutoka Tanzania Bara.....	57
B:	Wajumbe Kumi kutoka Tanzania Zanzibar.....	58

**SHERIA YA MABADILIKO YA KATIBA
(SURA 83)**

KANUNI ZA BUNGE MAALUM, 2014

[Zimetungwa Chini ya Kifungu cha 26(1)]

**SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI**

Jina 1.(1) Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Bunge Maalum, Toleo la mwaka 2014.

(2) Kanuni hizi zitaanza kutumika baada ya kupitishwa na Bunge Maalum.

Matumizi 2.(1) Bila kuathiri masharti ya Sheria, Kanuni hizi zitatumika kwa mambo yote yanayohusu utaratibu wa uendeshaji wa Shughuli za Bunge Maalum.

(2) Iwapo jambo au shughuli yoyote haikuwekewa masharti katika Kanuni hizi, Mwenyekiti ataamua utaratibu wa kufuata katika jambo au shughuli hiyo, kwa kuzingatia mila na desturi za uendeshaji wa Shughuli za Bunge Maalum.

(3) Utaratibu utakaowekwa kwa mujibu wa fasili ya (2) utatumika kama sehemu ya Kanuni hizi katika kuongoza uendeshaji wa Shughuli za Bunge Maalum

Tafsiri 3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama maelezo yanahitaji vinginevyo-
“**Akidi**” ni idadi ya Wajumbe wa Bunge Maalum inayoruhusiwa kufanya maamuzi ya Bunge Maalum kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 33(1) ya Kanuni hizi;

“**Bunge Maalum**” maana yake ni Bunge Maalum lililoundwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 22(1) cha Sheria;

“**Gazeti**” ni *Gazeti* la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

“**Hoja**” maana yake ni pendekezo mahsusi lililotolewa na Kamati ya Bunge Maalum au Mjumbe wa Bunge Maalum kwa ajili ya kupata Uamuzi wa Bunge Maalum kuhusu kuboresha masharti ya Rasimu ya Katiba;

“**Jamhuri ya Muungano**” ni eneo lote lililokuwa ndani ya mipaka ya Jamhuri ya Tanganyika na eneo lote lililokuwa ndani ya mipaka ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar kabla ya tarehe 26 Aprili, 1964;

“**Kamati**” ni Kamati yoyote ya Bunge Maalum iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni hizi;

“Kamati inayopendekezwa” maana yake ni Rasimu ya Katiba iliyopitishwa na Bunge la Katiba kwa ajili ya kupigiwa kura ya maoni.

“Katibu” ni Katibu wa Bunge Maalum au Naibu Katibu wa Bunge Maalum aliyetajwa katika Kifungu cha 24(1) cha Sheria na inajumisha pia mtumishi mwingine yeyote wa Bunge Maalum aliyeidhinishwa kutekeleza kazi ya Katibu;

“Kikao” ni kikao cha siku moja cha Bunge Maalum kinachianza kwa kusomwa Dua na kumalizika kwa kuahirisha Bunge Maalum hadi siku itakayotajwa;

“Kitabu cha Maamuzi” ni kitabu cha Kumbukumbu ya maamuzi mbalimbali ya Mwenyekiti kuhusu suala lolote la utaratibu katika Bunge Maalum;

“Maeneo ya Bunge” linajumuisha eneo lote la Ukumbi unaotumika kuendesha Mikutano ya Bunge Maalum, pamoja na ofisi, vyumba, maeneo ya mahojiano baina ya Wajumbe wa Bunge Maalum na watu wengine, kumbi, bustani, viwanja na maeneo yote mengine yanayotumiwa kuendesha shughuli za Bunge Maalum na Kamati zake;

“Mamlaka ya Bunge” ni mamlaka ya Bunge Maalum kama yalivyotajwa katika kifungu cha 25 cha Sheria;

“Maisha ya Bunge Maalum” ni muda wote unaoanzia tarehe ambapo Bunge Maalum limeitishwa na Rais likutane kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 22(4) na kuishia tarehe ya kuvunjwa kwake kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 28 cha Sheria;

“Mgeni” maana yake ni mtu yeyote ambaye si Mjumbe, Katibu au mtumishi yeyote wa sekretarieti ya Bunge Maalum, na ambaye hatekelezi kazi rasmi zinazohusu Bunge Maalum;

“Mjumbe” ni mtu aliyeteuliwa kuwa Mjumbe wa Bunge Maalum kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 22 cha Sheria;

“Mkutano wa Bunge” ni mfululizo wa vikao vya Bunge kuanzia kikao cha kwanza hadi cha mwisho, vinavyopangwa kwa ajili ya Bunge Maalum kujadili na kufanya uamuzi kuhusu jambo au hoja mahsusi iliyowekwa kwenye Orodha ya Shughuli kwa kuzingatia ratiba ya Shughuli za Bunge Maalum iliyowekwa kwa mujibu wa Kanuni hizi;

“Mpambe wa Bunge Maalum” ni mtumishi wa Seretarieti ya Bunge Maalum anayetekeleza majukumu yaliyoainishwa katika Kanuni ya 27 ya Kanuni hizi;

“Mwenyekiti” maana yake ni Mjumbe wa Bunge Maalum aliyechaguliwa kuwa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum kwa mujibu wa kifungu cha 23 cha Sheria;

“Mwenyekiti wa Kamati” maana yake ni mjumbe yeyote aliyechaguliwa kuongoza Kamati au Kamati Ndogo ya Kamati ya Bunge Maalum;

“Mwenyekiti wa Muda” maana yake ni mjumbe wa Bunge Maalum aliyechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa muda kwa mujibu wa Kifungu cha 22A cha Sheria;

“Mwenyekiti wa Tume” maana yake ni Mwenyekiti wa Tume ya Kuratibu na Kukusanya Maoni ya Wananachi kuhusu mchakato wa mabadiliko ya Katiba;

“Orodha ya Shughuli” ni Waraka mahsusi unaoonyesha mpangilio wa Shughuli za Bunge Maalum katika kila kikao cha Bunge Maalum;

“Rais” ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

“Rasimu ya Katiba” maana yake ni Rasimu ya Katiba ambayo imetayarishwa na Tume chini ya Sheria;

“Sekretarieti” ni watumishi wa Sekretarieti ya Bunge Maalum waliochaguliwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 24(5) na (6) cha Sheria;

“Sheria” maana yake ni Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83;

“Siwa” ni alama maalum inayotumika kama kielelezo cha mamlaka ya Bunge Maalum;

“Taarifa Rasmi” ni taarifa za majadiliano ya Bunge Maalum zilizotajwa kwenye Kanuni hizi;

“Tume” maana yake ni Tume iliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi kuhusu mchakato wa mabadiliko ya Katiba;

“Wimbo wa Taifa” ni wimbo wa Taifa wa Jamhuri ya Muungano.

SEHEMU YA PILI

HAKI, KINGA NA MADARAKA YA BUNGE MAALUM

Bunge
Maalum

4.(1) Bunge Maalum litaitishwa na Rais baada ya kukubaliana na Rais wa Zanzibar kupitia Tangazo kwenye *Gazeti* la Serikali ambalo litataja tarehe, siku, mahali na muda ambao Rais ameliitisha Bunge Maalum kukutana.

(2) Bunge Maalum litakuwa na Wajumbe watakaotangazwa na Rais kupitia agizo katika *Gazeti* la Serikali ambao ni-

- (a) Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- (b) Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar;
- (c) Wajumbe mia mbili na moja walioteuliwa na Rais kwa makubaliano na Rais wa Zanzibar kama ifuatavyo:
 - (i) Wajumbe ishirini kutoka Taasisi zisizokuwa za kiserikali;
 - (ii) Wajumbe ishirini kutoka Taasisi za kidini;
 - (iii) Wajumbe arobaini na mbili kutoka Vyama vyote vya siasa vyenye usajili wa kudumu;
 - (iv) Wajumbe ishirini kutoka Taasisi za elimu ya juu;
 - (v) Wajumbe ishirini kutoka makundi ya watu wenye ulemavu;
 - (vi) Wajumbe kumi na tisa kutoka Vyama vya Wafanyakazi;
 - (vii) Wajumbe kumi kutoka Vyama vya Wafugaji;
 - (viii) Wajumbe kumi kutoka Vyama vinavyowakilisha Wavuvi;
 - (ix) Wajumbe ishirini kutoka Vyama vya Wakulima;
 - (x) Wajumbe ishirini kutoka makundi mengine yoyote ambayo yana malengo yanayofanana.

Mamlaka
ya Bunge
Maalum

5.(1) Kwa mujibu wa kifungu cha 25 cha Sheria, Bunge Maalum litakuwa na mamlaka ya-

- (a) kujadili na kupitisha Rasimu ya Katiba; na
- (b) kutunga masharti ya mpito na masharti yatokanayo na Rasimu ya Katiba kadri litakavyoona inafaa.

(2) Katika kutekeleza mamlaka yake kwa mujibu wa fasili ya (1), Bunge Maalum litazingatia masharti ya Sheria na Kanuni hizi.

Haki na
kinga za
Bunge
Maalum

6.(1) Kutakuwa na uhuru wa mawazo, maoni katika mijadala ya Bunge Maalum na maoniya Mjumbe hayatahojiwa mahakamani au sehemu yoyote nje ya Bunge Maalum.

(2) Utaratibu wa kuendesha mijadala katika Bunge Maalum utakuwa kama ulivyowekwa na Kanuni hizi.

(3) Bila kuathiri masharti ya Sheria na Kanuni hizi, kila mjumbe wa Bunge Maalum atatekeleza majukumu yake kwa uhuru, na hatashurutishwa, hatashinikizwa wala kupokea maelekezo kutoka kwa mtu au chombo chochote.

(4) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria au sheria nyingine yeyote, Mjumbe yeyote hatashtakiwa au kufunguliwa shauri la madai mahakamani kutokana na jambo lolote alilolisema au kulifanya ndani ya Bunge Maalum linalohusiana na utekelezaji wa mamlaka ya Bunge Maalum.

(5) Mjumbe yeyote wa Bunge Maalum hatashitakiwa wala kufunguliwa shauri la madai mahakamani kutokana na jambo lolote alilolisema au alilolifanya katika kutekeleza uamuzi wowote wa Bunge Maalum au wa Kamati yoyote ya Bunge Maalum.

(6) Mjumbe yeyote wa Bunge Maalum hatakamatwa kwa sababu ya shauri lolote la madai, isipokuwa kwa kosa la jinai, ambapo Bunge Maalum litakuwa na haki ya kutaarifiwa kuhusu kukamatwa huko na sababu zake.

Ukomo
wa
mamlaka
ya Bunge
Maalum

7. Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 28(2) cha Sheria, Bunge Maalum litafikia ukomo wake baada ya kupitisha masharti ya Rasimu ya Katiba, masharti ya mpito na masharti yatokanayo na Rasimu ya Katiba.

SEHEMU YA TATU

MIKUTANO NA VIKAO VYA BUNGE MAALUM

Utaratibu wa
ukaaji ndani
ya Ukumbi
wa Mikutano
ya Bunge
Maalum

8.(1) Kila Mjumbe wa Bunge Maalum kabla ya kuingia katika Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum, na kukaa mahala pake, atatakiwa kuweka saina katika Kitabu cha Mahudhurio kitakachowekwa kwenye eneo litakalopangwa kwa ajili hiyo.

(2) Baada ya kuingia Ukumbini, kila Mjumbe atakaa mahala pake, kwa

mujibu wa utaratibu maalum wa ukaaji wa Wajumbe ndani ya Ukumbi wa Mikutano utakaokuwa umewekwa na Katibu.

(3) Wapambe na Watumishi wa Bunge Maalum pamoja na waandishi wa habari watakaa sehemu ambazo zimetengwa kwa ajili yao.

(4) Wageni wengine wanaweza kutengewa sehemu maalum ya kukaa.

(5) Wageni mashuhuri, Mabalozi na Viongozi wengine watakaa sehemu maalum kama itakavyopangwa na Katibu.

Mkutano wa
kwanza wa
Bunge
Maalum

9.(1) Mkutano wa kwanza wa Bunge Maalum utanza tarehe, siku na mahali ambapo Rais ataagiza kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 22(4) cha Sheria.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni hizi kuhusu kuanza na kukoma kwa vikao vya Bunge Maalum, Mkutano wa kwanza wa Bunge utaendelea kwa muda wowote ambao utahitajika kwa ajili ya kutekeleza na kukamilisha shughuli zote za Mkutano wa kwanza wa Bunge Maalum.

(3) Kila Mkutano unaofuata wa Bunge Maalum utanza siku yoyote itakayopangwa na Bunge lenyewe au siku yoyote itakayopangwa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Shughuli
za Mkutano
wa Kwanza
wa Bunge
Maalum

10.(1) Shughuli za Mkutano wa Kwanza wa Bunge Maalum zitakuwa kama ifuatavyo-

- (a) kusomwa kwa Tangazo la Rais la kuitisha Bunge Maalum;
- (b) uchaguzi wa Mwenyekiti wa muda;
- (c) kuandaa na kupitisha Kanuni za Uendeshaji wa Shughuli za Bunge Maalum;
- (d) uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti;
- (e) kiapo cha Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti;
- (f) wimbo wa Taifa na Dua ya Kuiombea Nchi na Bunge Maalum;
- (g) kiapo cha Wajumbe wa Bunge Maalum;
- (h) Uwasilishaji wa Rasimu ya Katiba;
- (i) shughuli yoyote nyingine ambayo Bunge Maalum litaona inafaa kufanywa au kutekelezwa kwa wakati huo.

(2) Mwanzoni mwa kikao cha kwanza cha Mkutano wa Kwanza wa Bunge Maalum, Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano au Katibu wa Baraza la Wawakilishi, atasoma Tangazo la Rais la kuliitisha Bunge Maalum.

(3) Mara baada ya Tangazo la Rais kusomwa kwa mujibu wa fasili ya (2), Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa pamoja watasimamia uchaguzi wa Mwenyekiti wa Muda wa Bunge Maalum kwa utaratibu watakaona kuwa unafaa.

(4) Baada ya Mwenyekiti wa Muda kupatikana, Bunge Maalum litafanya shughuli ya kuandaa na kupitisha Kanuni za Bunge Maalum zinazoweka utaratibu wa kuendesha shughuli zake.

(5) Bila ya kujali masharti ya fasili ya (6), Kanuni zilizopitishwa kwa mujibu wa fasili ya (4) zitaanza kutumika mara moja kuendesha Shughuli za Bunge Maalum, baada ya nakala zake kugawanywa kwa Wajumbe.

(6) Toleo la Kanuni za Bunge Maalum litachapishwa kwenye *Gazeti* la Serikali.

Utaratibu wa
kumchagua
Mwenyekiti
na Makamu
Mwenyekiti

11.(1) Kutakuwa na Uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum utakaofanyika katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge Maalum, mara baada Bunge Maalum kuandaa na kupitisha Kanuni zake.

(2) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti watachaguliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Bunge Maalum, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 23(4) cha Sheria na utaratibu ulioainishwa katika Nyongeza ya Kwanza ya Kanuni hizi.

(3) Uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti utafanyika na kuendeshwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 23 cha Sheria, masharti ya Kanuni hizi, na pia kwa kuzingatia utaratibu wa Uchaguzi uliowekwa na Nyongeza ya Kwanza ya Kanuni hizi.

(4) Endapo ikitokea kuwa Kiti cha Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti ki-wazi, uchaguzi utaitishwa kumchagua **Mjumbe** wa kuziba nafasi hiyo, na **Mjumbe** huyo atatakiwa atoke upande wa Jamhuri ya Muungano alikokuwa ametokea mtangulizi wake.

Kiapo cha
Mwenyekiti
na Makamu
Mwenyekiti

12.(1) Mjumbe yeyote aliyechaguliwa kuwa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti, kabla ya kushika madaraka yake, ataapa au kula yamini, vyovyote itakavyokuwa, mbele ya Katibu wa Bunge Maalum, kwa kutamka maneno yafuatayo yaliyowekwa na Jedwali la Nne la Sheria:

“Mimi.....nikiwa nimechaguliwa kuwa Mwenyekiti/Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum, naapa/nathibitisha kwamba nitakuwa mwaminifu na mtiifu kwa Jamhuri ya Muungano na kwa kadri ya uwezo na ufahamu wangu, nitatimiza wajibu wangu na kufanya kazi zinazonihusu bila upendeleo, na bila ya kukiuka Sheria za Nchi. Ewe Mungu nisaidie”.

(2) Wakati wa kuapa au kula yamini, Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti anayeamini kuwa kuna Mungu, atalazimika kushika Biblia au Kuran au kitabu kingine kitakatifu kinachotambuliwa na imani ya dini yake.

(3) Iwapo Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti haamini kuwa kuna Mungu, basi hatashika Biblia au Kuran au kitabu chochote kitakatifu au kutamka maneno “Ewe Mungu nisaidie”, bali atalazimika kuinua juu mkono wake wa kuume.

Wimbo wa
Taifa

13.(1) Baada ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kushika madaraka yao, Wimbo wa Taifa utapigwa na kuimbwa kuashiria kuanza rasmi kwa Shughuli za Bunge Maalum, na pia baada ya kikao cha mwisho cha Mkutano wa mwisho, kuashiria kukamilika kwa Shughuli za Bunge Maalum.

(2) Wakati Wimbo wa Taifa unapigwa na kuimbwa, kila Mjumbe na mtu yeyote aliyopo ndani ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum, atasimama mahala pake kwa staha na utulivu, kama ilivyo mila na desturi ya kutoa heshima kwa Wimbo wa Taifa unapopigwa na kuimbwa.

Dua ya
kuiombea
Jamhuri ya
Muungano
na Bunge
Maalum

14.(1) Dua ya kuiombea Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuliombea Bunge Maalum itasomwa na Mwenyekiti, itakuwa na maneno yafuatayo:-

“Ewe MWENYEZI MUNGU Mtukufu, Muumba Mbingu na Dunia, umeweka Mataifa katika Dunia, ili haki yako itendeke. Twakuomba uibariki Jamhuri ya Muungano wa Tanzania idumishe uhuru, umoja, haki na amani.

Utujalie hekima na busara, sisi Wajumbe wa Bunge hili Maalum ili tuwe na uwezo wa kujadili kwa dhati mambo yatakayoletwa mbele yetu leo, na kufanya maamuzi sahihi kwa manufaa ya watu wote na ustawi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Amina.”

(2) Wakati Dua ya kuiombea Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuliombea Bunge Maalum itakapokuwa inasomwa, kila Mjumbe aliyepo ndani ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum atasimama kwa staha na utulivu mahala pake, kama ilivyo mila na desturi ya kutoa heshima kwa Dua.

Kiapo kwa
Mjumbe wa
Bunge
Maalum

15.(1) Kila Mjumbe ataapa au kula yamini mbele ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti kwa kutamka maneno yafuatayo:

“Mimi nikiwa nimeteuliwa kuwa Mjumbe wa Bunge Maalum, naapa/nathibitisha kwamba nitakuwa mwaminifu na mtiifu kwa Jamhuri ya Muungano na kwa kadri ya uwezo na ufahamu wangu, nitatimiza wajibu wangu na kufanya kazi zinazonihusu bila ya upendeleo, na bila ya kukiuka Sheria za nchi. Ewe Mungu Nisaidie.”

(2) Wakati wa kuapa au kula yamini, Mjumbe anayeamini kuwa kuna Mungu, atalazimika kushika Biblia au *Kuran* au kitabu kingine kitakatifu kinachotambuliwa na imani ya dini yake.

(3) Iwapo Mjumbe haamini kuwa kuna Mungu, basi hatahika Biblia au *Kuran* au kitabu chochote kitakatifu au kutamka maneno “*Ewe Mungu nisaidie*”, bali atalazimika kuinua juu mkono wake wa kuume.

(4) Utaratibu wa kuapa au kula yamini utakuwa ni kwa mujibu wa Orodha ya majina ya Wajumbe iliyoandaliwa kwa kuzingatia mpangilio wa alfabeti ya kwanza ya jina la kwanza la kila Mjumbe.

Mikutano ya
kawaida ya
Bunge
Maalum

16.(1) Isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo, kila Mkutano wa Bunge Maalum utafanyika katika Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum ulioandaliwa kwa ajili hiyo.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni zinazofuata za Kanuni hii, kila Mkutano, isipokuwa Mkutano wa Kwanza wa Bunge Maalum, utaanza siku, tarehe na wakati utakaowekwa na Bunge Maalum.

(3) Iwapo manufaa ya Taifa yatahitaji kuwa Bunge Maalum lisikutane tarehe ile iliyowekwa kwa Mkutano utakaofuata, bali likutane tarehe ya mbele zaidi au ya nyuma zaidi, basi Mwenyekiti anaweza, baada ya kushauriana na Kamati ya Shughuli za Bunge Maalum kuliitisha Bunge likutane tarehe hiyo ya mbele zaidi au nyuma zaidi.

Utaratibu wa
vikao vya
Bunge
Maalum

17.(1) Vikao vya Mikutano ya Bunge Maalum, isipokuwa kikao cha kwanza cha Mkutano wa Kwanza wa Bunge Maalum, vitaanza saa tatu asubuhi, ila tu kama Bunge Maalum litaamua vinginevyo.

(2) Bunge Maalum litakutana hadi saa saba mchana ambapo Mwenyekiti atasitisha Shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika, hadi saa kumi jioni:

Isipokuwa kwamba, Mwenyekiti akiona inafaa, Bunge Maalum linaweza kuendelea kukutana kwa muda usiozidi dakika thelathini, au kusitishwa wakati wowote kabla ya saa saba mchana, baada ya kuwahoji Wajumbe.

(3) Hoja ya kubadilisha nyakati za vikao inaweza kutolewa na Mjumbe yeyote na itaamuliwa kama hoja nyingine yoyote na haitahitaji kutolewa taarifa.

(4) Bunge Maalum litaendelea kukutana hadi saa mbili usiku, wakati ambapo Mwenyekiti atasitisha shughuli na kuliahirisha hadi kesho yake au siku nyingine atakayoitaja.

(5) Endapo shughuli zilizopangwa kwa siku hiyo zimemalizika kabla ya saa mbili usiku, Mwenyekiti ataliahirisha Bunge Maalum bila kuhoji, lakini iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuliahirisha, na Bunge au Kamati ya Bunge Zima bado haijamaliza shughuli zake, Mwenyekiti anaweza kuongeza muda usiozidi dakika thelathini, bila kuhoji Bunge au Kamati ya Bunge Zima, ili kukamilisha shughuli zilizobaki.

(6) Iwapo wakati wa kusitisha Shughuli umefika na Mwenyekiti atakuwa analihoji au yupo karibu kulihoji Bunge Maalum, basi hatastitisha Shughuli hadi hoja iwe imeamuliwa, na baada ya hoja kuamuliwa, Mwenyekiti ataliahirisha Bunge Maalum hadi kesho yake au siku nyingine atakayoita.

(7) Endapo majadiliano yote ya Bunge Maalum au Kamati ya Bunge Zima yatasitishwa na Mwenyekiti kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hii, wakati yatakaporudiwa katika Bunge Maalum au katika Kamati ya Bunge Zima, yataendelezwa kuanzia pale yalipositishwa, na Mjumbe yeyote ambaye hotuba yake ilikatizwa na Mwenyekiti, atakuwa na haki ya kuendelea na maelezo yake katika marudio ya mjadala huo, na endapo Mjumbe hatoitumia haki yake hiyo, basi atahesabiwa kuwa alikuwa amemaliza kutoa maelezo yake.

(8) Iwapo shughuli zilizopangwa kwa ajili ya kikao hazijamalizika, na mjumbe akatoa hoja ya kuahirisha kikao kutokana na dhamira au sababu nyingine yoyote. Mwenyekiti atalihoji Bunge Maalum kuhusu hoja ya kuahirisha kikao hicho na baada ya hoja hiyo kuafikiwa, atakiahirisha kikao hicho hadi kikao kinachofuata ambacho, kama Bunge Maalum halikuamua vinginevyo, kitakuwa ni siku itakayofuata, isipokuwa tu kama itakuwa ni siku ya Jumamosi, Jumapili au siku ya mapumziko.

Kuahirisha
Mkutano wa
Bunge
Maalum

18.(1) Isipokuwa kwa Mkutano wa mwisho wa Bunge Maalum, kila Mkutano wa Bunge Maalum utafungwa kwa kuliahirisha Bunge Maalum hadi Mkutano utakaofuata.

(2) Endapo Shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli kwa ajili ya Mkutano huo zimemalizika, Mwenyekiti atalihoji Bunge Maalum kuhusu hoja ya kuahirisha Bunge Maalum.

(3) Mara tu baada ya Bunge Maalum kupitisha hoja ya kuahirisha Mkutano wa Bunge Maalum, Mwenyekiti ataliahirisha Bunge Maalum hadi siku, muda na mahali atakapopataja:

Isipokuwa kwamba, iwapo kikao hicho kitakuwa ni cha mwisho cha Mkutano wa Mwisho wa Bunge Maalum, Wimbo wa Taifa utapigwa na kuimbwa kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Kanuni hizi.

Wajibu wa
Mjumbe
kuhudhuria
Mikutano na

19.(1) Kila Mjumbe wa Bunge Maalum atakuwa na wajibu wa kuhudhuria Mikutano na vikao vyote vya Bunge Maalum na Kamati zake.

vikao vya
Bunge
Maalum

(2) Mjumbe yeyote atakayepata tatizo lolote linalomfanya ashindwe kuhudhuria Mkutano au kikao cha Bunge Maalum na Kamati zake, atatakiwa kumwarifu na kumwomba ruhusa Mwenyekiti wa Bunge Maalum na pia Mwenyekiti wa Kamati husika ya Bunge Maalum kwa maandishi.

(3) Mjumbe yeyote ambaye atashindwa kuhudhuria kikao chochote cha Bunge Maalum hatalipwa posho ya kikao au vikao alivyoshindwa kuhudhuria.

(4) Kwa kuzingatia kwamba, kuhudhuria Mikutano na vikao vya Bunge Maalum na Kamati zake ni wajibu wa kwanza wa kila Mjumbe, mtu au chombo chochote kitakachomkamata na kumzuia Mjumbe yeyote wa Bunge Maalum kuhudhuria Mikutano na vikao vya Bunge Maalum kitalazimika kutoa taarifa ya maandishi kwa Mwenyekiti kuhusu kukamatwa na kuzuliwa kwa Mjumbe huyo na sababu zake.

SEHEMU YA NNE

UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA BUNGE MAALUM

(a) Viongozi wa Bunge Maalum

Mwenyekiti
na mamlaka
yake

20.(1) Mwenyekiti atakuwa ndiye kiongozi wa Bunge Maalum, na majukumu yake yatakuwa ni:

- (a) kuongoza Mikutano na vikao vya Bunge Maalum;
- (b) kuongoza mwenendo na utaratibu wa majadiliano katika Mikutano na vikao vya Bunge Maalum;
- (c) kutoa uamuzi kuhusu masuala yote ya utaratibu katika Mikutano na vikao vya Bunge Maalum;
- (d) kusimamia amani na utulivu katika Mikutano na vikao vya Bunge Maalum;
- (e) kusimamia uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge Maalum.

(2) Mwenyekiti wa Bunge Maalum atakuwa na madaraka na mamlaka ya kutafsiri Kanuni hizi, na uamuzi wake kuhusu suala lolote la utaratibu kwa mujibu wa Kanuni hizi utakuwa ni wa mwisho.

(3) Katika kutekeleza majukumu yake, Mwenyekiti ataongozwa na Sheria pamoja na Kanuni hizi, na pale ambapo Kanuni hazikutoa mwongozo, basi ataongozwa na sheria nyingine za nchi, kanuni nyingine zilizopo, pamoja na mila na desturi za nchi nyingine katika uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge Maalum.

(4) Mwenyekiti atawajibika kusimamia ipasavyo Kanuni zote za Bunge Maalum, na katika kutekeleza wajibu huo, anaweza kumtaka Mjumbe

yeyote anayekiuka Kanuni yeyote au utaratibu uliowekwa na Kanuni hizi ajirekebishe mara moja.

(5) Bila ya kujali masharti ya fasili ya (3), wakati wowote ambapo Mwenyekiti hatakuwepo katika Bunge Maalum, au kwa sababu nyingine yoyote hawezi kutekeleza madaraka na majukumu ya Mwenyekiti, basi madaraka na majukumu hayo yatatekelezwa na Makamu Mwenyekiti.

(6) Mwenyekiti atakoma kuwa Mwenyekiti na Kiti cha Mwenyekiti kitakuwa ki-wazi endapo litatokea tukio lolote kati ya matukio yafuatayo-

- (a) atafariki;
- (b) atajiuzulu;
- (c) atathibitika kuwa amekosa uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa sababu za kiafya;
- (d) atatiwa hatiani kwa kosa ambalo adhabu yake ni kifungo gerezani kwa muda usiopungua mwezi mmoja; na
- (e) atapoteza sifa ya kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Bunge Maalum.

(7) Hakuna shughuli yoyote itakayotekelezwa katika Bunge Maalum wakati wowote ambapo Kiti cha Mwenyekiti kitakuwa ki-wazi, isipokuwa uchaguzi wa Mwenyekiti.

Makamu
Mwenyekiti
na
majukumu

21.(1) Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum atashika madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Sheria na Kanuni hizi.

(2) Makamu Mwenyekiti atakuwa msaidizi wa Mwenyekiti katika kuliongoza Bunge Maalum na atatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi.

(3) Wakati wowote ambao Mwenyekiti hayupo katika Bunge au kwa sababu nyingine yoyote hawezi kutekeleza mamlaka na majukumu yake, basi mamlaka au majukumu hayo yatatekelezwa na Makamu Mwenyekiti.

(4) Wakati wowote ambao Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wote hawapo Bungeni, au kwa sababu nyingine yoyote hawawezi kutekeleza mamlaka na majukumu yao, basi mamlaka na majukumu hayo yatatekelezwa na Mjumbe yeyote atakayechaguliwa na Wajumbe kwa ajili hiyo.

(5) Makamu Mwenyekiti atakoma kuwa Makamu Mwenyekiti na Kiti cha Makamu Mwenyekiti kitakuwa ki-wazi iwapo -

- (a) atafariki;

- (b) atajiuzulu,
- (c) atathibitika kuwa amekosa uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa sababu za kiafya;
- (d) atatiwa hatiani kwa kosa ambalo adhabu yake ni kifungo gerezani kwa muda usiopungua mwezi mmoja; na
- (e) atapoteza sifa ya kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Bunge Maalum.

Uadilifu kwa
viongozi wa
Bunge
Maalum

22.(1) Kwa kuzingatia kiapo cha kazi yake kilichowekwa kwa mujibu wa Sheria, na kwa madhumuni ya uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge Maalum, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mjumbe yeyote atakayekuwa amechaguliwa kutekeleza kazi na majukumu ya Mwenyekiti wa Bunge Maalum, ataendesha Shughuli za Bunge Maalum kwa kutoa uamuzi kwa haki, kwa uadilifu na bila chuki wala upendeleo wowote, kwa kuongozwa na Sheria, sheria nyingine za nchi, Kanuni hizi, Kanuni nyingine zilizopo, pamoja na mila na desturi za Nchi nyingine katika uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge Maalum.

Katibu na
Naibu
Katibu wa
Bunge
Maalum

23. Katibu na Naibu Katibu wa Bunge Maalum kama walivyotajwa katika kifungu cha 24 cha Sheria, kabla ya kushika madaraka yao, kila mmoja wao ataapishwa na Rais kiapo kilichowekwa kwa mujibu wa kifungu cha 24(7) cha Sheria.

Kazi na
majukumu
ya Katibu wa
Bunge
Maalum

24.(1) Katibu atawajibika kuhakikisha utekelezaji bora wa kazi na majukumu ya Bunge Maalum, na kwa madhumuni hayo-

- (a) atahudhuria au atawakilishwa na mtumishi yeyote wa Bunge Maalum katika vikao vyote vya Bunge Maalum, vikao vya Kamati ya Bunge Zima, na vikao vya Kamati nyingine yoyote ya Bunge Maalum;
- (b) ataweka kumbukumbu zote zinazotakiwa ziwekwe kwa mujibu wa Kanuni hizi;
- (c) atatayarisha Taarifa Rasmi za majadiliano ya Bunge Maalum kwa mujibu wa Kanuni hizi;
- (d) atatayarisha kwa utaratibu wa siku hadi siku, kitabu cha Shughuli za Bunge Maalum na kukihifadhi ofisini kikiwa kinaonesha yafuatayo:
 - (i) maagizo yeyote yaliyotolewa na Bunge Maalum;
 - (ii) shughuli zote zilizopangwa kufanywa siku yoyote ya baadaye; na
 - (iii) taarifa zote za hoja zilizokubaliwa na Mwenyekiti.

(2) Katibu atawajibika kuhakikisha utekelezaji bora wa Shughuli za Bunge Maalum na kwa madhumuni hayo atatayarisha siku hadi siku, Orodha ya Shughuli za Bunge Maalum kama itakavyoelekezwa na Mwenyekiti.

(3) Katibu atawajibika kutunza kitabu cha Maamuzi ya Mwenyekiti, Kitabu cha Shughuli, Taarifa Rasmi za Majadiliano ya Bunge Maalum, nakala ya Rasimu ya Katiba, nakala ya Katiba, unayopendekezwa na Bunge Maalum na hati nyingine zilizowasilishwa katika Bunge Maalum.

(4) Mwananchi yeyote anaweza kukagua kumbukumbu zilizoinishwa katika fasili ya (3) wakati wowote unaofaa kwa kufuata utaratibu utakaowekwa na Mwenyekiti.

(5) Katibu ataweka kumbukumbu ya Uamuzi wa mara kwa mara wa Mwenyekiti kuhusu masuala ya utaratibu katika Bunge Maalum.

(6) Katibu atawajibika kuhakikisha kuwa Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum, Kumbi za Mikutano ya Kamati za Bunge Maalum, maeneo ya Bunge Maalum, huduma kwa Wajumbe wa Bunge Maalum na vifaa vingine vinavyohusika na Shughuli za Bunge Maalum viko katika hali nzuri na inayofaa kuliwezesha Bunge Maalum kutekeleza kazi na majukumu yake ipasavyo.

Naibu
Katibu na
majukumu
yake

25.(1) Naibu Katibu atashika madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Sheria na Kanuni hizi.

(2) Naibu Katibu atakuwa msaidizi wa Katibu katika kuhakikisha utekelezaji bora wa kazi na majukumu ya Bunge Maalum, na katika utekelezaji wa kazi na majukumu ya Ofisi ya Katibu.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria na Kanuni hizi, wakati wowote ambao Katibu hatakuwepo au kwa sababu nyingine yoyote hawezi kutekeleza madaraka na majukumu yake, basi madaraka na majukumu hayo yatatekelezwa na Naibu Katibu.

(4) Endapo wakati wowote Katibu na Naibu Katibu wote hawapo Bungeni, au kutokana na sababu nyingine yoyote, hawawezi kutekeleza madaraka na majukumu yao, basi madaraka na majukumu hayo yatatekelezwa na mtumishi yoyote wa Bunge Maalum atakayeteuliwa na Katibu kwa ajili hiyo.

(b) Sekretarieti ya Bunge Maalum

Sekretarieti
ya Bunge
Maalum

26.(1) Katibu na Naibu Katibu wa Bunge Maalum, watateua watumishi kuunda Sekretarieti ya Bunge Maalum, kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 24 cha Sheria.

(2) Sekretarieti ya Bunge Maalum itakuwa na watumishi kwa idadi na nafasi za madaraka ambazo Katibu na Naibu Katibu wa Bunge Maalum wataona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi na majukumu ya Bunge Maalum.

(3) Sekretarieti ya Bunge Maalum chini ya uongozi wa Katibu na Naibu wa Bunge Maalum itatekeleza kazi na shughuli zote zilizowekwa au zitakazokuwa ni muhimu kwa ajili ya kuhakikisha utekelezaji bora wa shughuli za Bunge Maalum kwa mujibu wa masharti ya Sheria na ya Kanuni hizi.

(c) Uendeshaji wa Shughuli

Shughuli za
kila siku

27.(1) Katibu ataandaa Orodha ya Shughuli za kila siku za vikao vya Bunge Maalum, kwa mujibu wa maelekezo ya Mwenyekiti baada ya kushauriana na Kamati ya Shughuli na kugawa nakala kwa kila Mjumbe kabla ya kikao husika.

(2) Katibu, kwa maelekezo ya Mwenyekiti, baada ya kushauriana na Kamati ya Shughuli za Bunge Maalum, anaweza kuandaa Nyongeza ya Orodha ya Shughuli, na kugawa nakala kwa kila Mjumbe, kabla au wakati wa kikao husika.

(3) Kamati ya Shughuli iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni hizi itamshauri Mwenyekiti kuhusu uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge Maalum.

Upangaji wa
muda wa
kutekeleza
shughuli

28.(1) Mwenyekiti kwa kushirikiana na Kamati ya Shughuli atapanga muda wa majadiliano ya Bunge kwa kila jambo litakalowasilishwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa.

(2) Baada ya muda uliopangwa kwa mujibu wa fasili ya (1) kuisha, Mwenyekiti baada ya kusitisha majadala, atalihoji Bunge kwa ajili ya kupata uamuzi kuhusu jambo lililokuwa linajadiliwa.

(d) Mpangilio wa Shughuli

Mpangilio
wa Shughuli
za Bunge
Maalum

29.(1) Shughuli za Bunge Maalum zitaendeshwa kwa kufuata mpangilio ufuatao:-

- (a) kuwaapisha Wajumbe wapya Kiapo cha Utii;
- (b) Taarifa ya Mwenyekiti;
- (c) mambo yanayohusu haki za Bunge, ikiwa ni pamoja na kuzifanyia marekebisho Kanuni za Bunge Maalum;
- (d) taarifa au hoja za Kamati;

(e) shughuli yoyote ambayo Bunge Maalum litaona inafaa kushughulikiwa kwa wakati huo.

(2) Shughuli za Bunge Maalum katika kila kikao zitatekelezwa kwa kufuata Orodha ya Shughuli za siku hiyo au kwa kufuata utaratibu mwingine ambao Mwenyekiti ataagiza ufuatwe kwa ajili ya uendesaji bora wa Shughuli za Bunge Maalum.

(3) Baada ya hoja yoyote kuwasilishwa na kujadiliwa, Bunge Maalum linaweza kuamua kuipitisha hoja hiyo kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Kanuni hizi, au kwamba, hoja hiyo ipelekwe kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika ili ifanyiwe kazi na kupata ushauri wa ziada kuhusu hoja hiyo kabla ya kuipitisha.

Taarifa ya
Mwenyekiti

30. Wakati wa kikao chochote cha Bunge Maalum, Mwenyekiti anaweza kutoa taarifa yoyote kuhusu Shughuli za Bunge Maalum kadri atakavyoona inafaa.

Mambo
yanayohusu
haki za
Bunge
Maalum

31.(1) Jambo lolote linalohusu haki za Bunge Maalum litawasilishwa kwa kufuata mpangilio wa Shughuli za Bunge uliowekwa chini ya Kanuni ya 30(1) ya Kanuni hizi, baada ya Mwenyekiti kuarifiwa mapema kuhusu jambo hilo.

(2) Endapo baada ya kupata taarifa mapema, Mwenyekiti ataamua kwamba jambo hilo liwasilishwe kwenye Bunge Maalum, basi atampa nafasi Mjumbe anayehusika kuliwasilisha kwa kutoa maelezo mafupi kuhusu jambo lenyewe na sababu zinazomfanya aamini kwamba linahusu haki za Bunge Maalum zilizotajwa kwenye Sheria na Kanuni hizi.

(3) Hoja inayohusu jambo linalohusu haki za Bunge Maalum itapewa kipaumbele katika mpangilio wa Shughuli nyingine zote zilizopangwa kwa kikao kinachohusika.

(4) Iwapo wakati wa kikao chochote cha Bunge Maalum jambo lolote linaloonekana linahusu haki za Bunge Maalum litazuka ghafla, Shughuli zitasitishwa kwa madhumuni ya kuliwezesha jambo hilo kuwasilishwa na kuamuliwa, isipokuwa tu kama wakati huo kura inapigwa.

(e) Uhalali wa Shughuli

Akidi ya
vikao vya
Bunge
Maalum

32.(1) Akidi kwa kila kikao cha Bunge Maalum, isipokuwa wakati wa kupitisha Uamuzi wa Bunge Maalum, itakuwa ni nusu ya Wajumbe wote wa Bunge Maalum.

(2) Mjumbe yeyote aliyehudhuria anaweza kumjulisha Mwenyekiti kwamba, Wajumbe waliopo ni pungufu ya akidi inayohitajika kwa ajili ya Shughuli inayoendelea.

(3) Endapo Mwenyekiti ataridhika kwamba, idadi ya Wajumbe walio ndani ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge ni pungufu ya akidi inayohitajika, basi atasitisha Shughuli za Bunge kwa muda atakaoutaja na atamwagiza Katibu kupiga kengele.

(4) Bunge Maalum litakaporejea baada ya muda uliotajwa chini ya fasili ya (3) kukamilika, Mwenyekiti atahakiki kama idadi ya Wajumbe waliopo inafikia akidi inayohitajika ili kuwezesha Shughuli inayohusika kuendelea.

(5) Endapo Mwenyekiti ataridhika kwamba bado idadi ya Wajumbe waliomo ndani ya Ukumbi wa Bunge haifikii akidi inayohitajika, basi ataahirisha Shughuli inayohusika ya Bunge hadi muda mwingine atakaoutaja.

(6) Shughuli za Bunge Maalum pamoja na Uamuzi wowote wa Bunge Maalum hautakuwa batili kwa sababu tu kwamba nafasi yoyote ya Mjumbe ipo wazi.

(f) Utaratibu wa Kujadili Hoja

Utaratibu wa
kujadili hoja

33. Mjumbe wa Bunge Maalum atakapoitwa na Mwenyekiti kujadili hoja, atasimama mahali pake na kutoa maelezo yake, kwa kuyaelekeza kwa Mwenyekiti.

Kubadilisha
hoja

34.(1) Hoja ikishatolewa ili iamuliwe inaweza kubadilishwa kwa:-

- (a) kuondoa maneno fulani kwa ajili ya kuingiza maneno mengine;
- (b) kuondoa maneno fulani bila ya kuongeza mengine;
- (c) kuingiza au kuongeza maneno mapya.

(2) Hoja ya marekebisho au mabadiliko ya hoja yoyote, itawasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Maalum inayohusika, na endapo haitapitishwa kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi, hoja hiyo itatenguka na Katibu ataweka kumbukumbu kwenye Taarifa Rasmi kwamba, kwakuwa hoja au marekebisho au mabadiliko hayo hayakuungwa mkono, basi hayakujadiliwa.

(3) Iwapo hoja ya mabadiliko inapendekeza kuondoa maneno fulani na kuingiza maneno mengine, basi mjadala juu ya suala la kufanya mabadiliko unaweza kuangalia kwa pamoja yale maneno yanayopendekezwa yaondolewe na maneno ambayo yanapendekezwa yaingizwe.

(4) Iwapo hoja inapendekeza kuondoa au kuingiza maneno, mjadala utahusu tu uondoaji au uingizaji wa maneno mapya, kadiri itakavyokuwa.

(5) Hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja nyingine ya mabadiliko sharti ihusiane na hoja ya kwanza ya mabadiliko na itatolewa, itajadiliwa na kuamuliwa kabla ya ile hoja ya kwanza ya mabadiliko kufanyiwa uamuzi.

Mabadiliko
ya hoja na
kuondoa
hoja ya
mabadiliko

35.(1) Endapo Kamati inataka kupendekeza mabadiliko yafanywe katika hoja kwa kufuata masharti ya Kanuni hizi, inaweza kutoa hoja yake ya kufanya mabadiliko wakati wowote baada ya hoja inayotaka kuibadilisha kutolewa, lakini kabla ya Bunge kuhojiwa liifanyie uamuzi.

(2) Endapo kuna mapendekezo mawili au zaidi ya kubadilisha hoja moja, Mwenyekiti ataweka utaratibu wa mpangilio atakaoona unafaa, lakini pia Mwenyekiti anaweza kuelekeza mapendekezo hayo yapelekwe na kujadiliwa kwanza kwenye Kamati iliyoshughulikia hoja hiyo.

(3) Iwapo mapendekezo yote ya mabadiliko yameamuliwa, Mwenyekiti ataitoa tena hoja ya awali ili ijadiliwe kama itakavyokuwa imebadilishwa.

(4) Hoja yoyote ya mapendekezo ya marekebisho au mabadiliko inaweza kuondolewa wakati wowote kabla haijafikishwa Bungeni iwapo Kamati inayotoa hoja itampelekea Katibu, taarifa ya maandishi ya kuiondoa hoja hiyo.

(5) Endapo hoja ya mapendekezo ya marekebisho ya mabadiliko imefikishwa Bungeni, Kamati inayotoa hoja hiyo inaweza tu kuiondoa hoja yake kwa Mwenyekiti wa Kamati husika kusimama mahali pake na kusema “*Ninaomba ruhusa kuondoa hoja*”, na papo hapo Mwenyekiti wa Bunge Maalum ataliuliza Bunge kama inafiki hoja hiyo kuondolewa na inapotokea Wajumbe walio wengi watakubali, Mwenyekiti atasema “*Hoja inaondolewa kwa idhini ya Bunge*” na hoja hiyo itakuwa imeondolewa, na Bunge litaendelea na Shughuli inayofuata.

SEHEMU YA TANO

KANUNI ZA MAJADILIANO

Nyakati za
Mjumbe
kusema
Bungeni

36. Kwa idhini ya Mwenyekiti wa Bunge Maalum, Mjumbe yeyote wa Bunge Maalum anaweza kusimama na kuchangia Bungeni katika nyakati zifuatazo:-

- (a) wakati wa kuchangia mjadala wa hoja yoyote iliyowasilishwa katika Bunge Maalum ambayo Kanuni zinaruhusu ijadiliwe;
- (b) wakati anawasilisha mabadiliko yoyote ya hoja;
- (c) wakati amesimama kutaka kuzungumzia jambo lolote linalohusu utaratibu;
- (d) wakati amesimama kuzungumzia jambo linalohusu haki za Bunge Maalum.

37.(1) Mjumbe yeyote akitaka kusema katika Bunge Malaum anaweza-

- (a) kumpelekea Mwenyekiti ombi kwa maandishi;
- (b) kusimama kimya mahali pake; au
- (c) kutumbukiza kadi ya elektroniki.

(2) Isipokuwa kwamba, Mjumbe yeyote hataanza kuzungumza hadi aitwe na Mwenyekiti kwa jina lake na kumruhusu kusema, na wakati wa kusema ataelekeza maneno yake kwa Mwenyekiti wa Bunge Maalum.

(3) Mjumbe akimaliza kutoa maelezo yake atakaa kwenye nafasi yake na hapo Mwenyekiti atamwita Mjumbe mwingine aliyepeleka ombi la maandishi au kama Mwenyekiti hakupata ombi lolote la maandishi, basi Mjumbe mwingine yeyote anayetaka kujadili hoja, anaweza kusimama mahali pake na kusubiri Mwenyekiti amwone.

(4) Iwapo Wajumbe wawili au zaidi watasimama wakati mmoja, Mwenyekiti atamwita Mjumbe atakayemwona kwanza.

(5) Endapo maombi ya kuchangia hoja fulani yatakuwa mengi zaidi ya muda uliotengwa kwa hoja hiyo, Mwenyekiti atatoa nafasi ya kwanza kwa Wajumbe ambao:-

- (a) hawajachangia katika hoja zilizotangulia kujadiliwa katika Mkutano unaoendelea; au
- (b) wamechangia mara chache katika hoja zilizotungulia kujadiliwa.

(6) Bila ya kuathiri masharti ya fasili ya (5) Mwenyekiti atahakikisha kuwa, nafasi za kuchangia zinatolewa kwa uwiano unaofaa baina ya aina zote za Wajumbe walioomba kuchangia hoja hiyo.

(7) Masharti yaliyotangulia katika Kanuni hii, hayatamzuia Mwenyekiti kutoa nafasi ya kuchangia kwa Mjumbe mwingine yeyote iwapo ataona kuwa, taaluma au uzoefu fulani wa Mjumbe huyo utaboresha hoja inayojadiliwa.

(8) Mjumbe hatasoma maelezo, isipokuwa, kwa madhumuni ya kutilia nguvu maelezo yake, anaweza kusoma dondoo kutoka kwenye kumbukumbu zilizoandikwa au kuchapishwa, na anaweza pia kujikumbusha kwa kuangalia kwenye kumbukumbu alizoziandika.

(9) Kila Mjumbe atazungumzia jambo ambalo liko katika mjadala tu na hatarudiarudia maneno yake au yale yaliyokwisha kusemwa na Wajumbe

wengine, na iwapo itatolewa hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja inayojadiliwa, mjadala sharti uhusu hoja hiyo ya mabadiliko mpaka imalizike, ndipo mjadala urudie kwenye hoja ya msingi.

(10) Kila Mjumbe atasema akiwa amesimama na atatoa maelezo yake kwa kutumia vyombo vilivyowekwa kwa madhumuni ya kutafsiri, kukuza na kurekodi sauti:

Isipokuwa, kwa ruhusa ya Mwenyekiti, Mjumbe yeyote aliye na ulemavu au ugonjwa anaweza kuzungumza akiwa ameketi.

(11) Endapo Mwenyekiti atasimama wakati Mjumbe yoyote anatoa hotuba ndani ya Bunge Maalum, au atakuwa amesimama mahali pake akisubiri kuanza kuzungumza, Mjumbe huyo ataketi mahali pake na Bunge Maalum litabaki kimya ili Mwenyekiti aweze kutoa maelekezo au taarifa yake.

(12) Mjumbe hataruhusiwa kuzungumzia hoja iliyokuwa likijadiliwa baada ya Mwenyekiti kuwahoji Wajumbe na hoja hiyo kutolewa uamuzi.

Mambo
yasiyoru-
husiwa
Bungeni

38.(1) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria na Kanuni hizi yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge Maalum, Mjumbe haruhusiwi:-

- (a) kusema uongo ndani ya Bunge Maalum;
- (b) kutoa ndani ya Bunge Maalum taarifa zisizokuwa na ukweli;
- (c) kuzungumzia jambo lolote ambalo halipo kwenye mjadala;
- (d) kuzungumzia jambo lolote ambalo limekwisha kutolewa uamuzi;
- (e) kutumia jina la Rais kwa dhihaka au kwa madhumuni ya kutaka kushawishi Bunge Maalum kuamua jambo lolote kwa namna fulani;
- (f) kuzungumzia mwenendo wa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti; isipokuwa tu kama imetolewa hoja mahsusi ya kumwondoa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti madarakani;
- (g) kumsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mwenyekiti, au Makamu Mwenyekiti, au Mjumbe au kwa mtu mwingine yeyote;
- (h) kutumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine;
- (i) kutoa kauli za dhihaka au zinazoshutumu mwenendo wa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti au Mjumbe au mtu mwingine yeyote;
- (j) kufanya jambo lolote ambalo linaathiri heshima ya Bunge Maalum au mwenendo bora wa Shughuli za Bunge;

(k) kufanya jambo lolote ambalo linakiuka masharti ya Sheria na Kanuni hizi.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya fasili ya (1), ni marufuku kwa Mjumbe kusema uongo ndani ya Bunge Maalum, na Mjumbe yeyote anapokuwa anasema Bungeni ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo ya ukweli kuhusu jambo analolizungumzia.

(3) Mjumbe yeyote anapokuwa akisema ndani ya Bunge Maalum hatachukuliwa kuwa anasema uongo iwapo anafanya rejea ya andiko la kitabu au utafiti kuhusu jambo fulani au habari kuhusu jambo hilo iliyotangazwa au iliyoandikwa na vyombo vya habari.

(4) Mjumbe mwingine yeyote anaweza kusimama mahali pake na kutamka “*kuhusu utaratibu*” na baada ya kuruhusiwa na Mwenyekiti kudai kwamba, Mjumbe aliyekuwa anasema kabla yake ametoa maelezo ya uongo kuhusu jambo au suala alilokuwa analisema Bungeni.

(5) Mjumbe anayetoa madai kwa mujibu wa fasili ya (4) ya Kanuni hii atakuwa na wajibu wa kutoa na kuthibitisha ukweli kuhusu jambo au suala hilo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge Maalum.

(6) Bila ya kuathiri masharti ya fasili zilizotangulia za Kanuni hii, Mwenyekiti au Mjumbe yeyote, baada ya kutoa maelezo mafupi ya ushahidi unaotilia mashaka ya dhahiri kuhusu ukweli wa kauli au usemi au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo Mjumbe amelisema ndani ya Bunge Maalum, anaweza kumdai Mjumbe huyo atoe uthibitisho wa ukweli wa kauli au maelezo yake na kama atashindwa kufanya hivyo, afute kauli au usemi au maelezo yake hayo.

(7) Mjumbe aliyetakiwa kuthibitisha ukweli wa kauli au maelezo yake aliyoyatoa katika Bunge Maalum, atawajibika kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge Maalum, papo hapo au katika muda atakaopewa na Mwenyekiti kwa ajili ya kufanya hivyo.

(8) Endapo Mjumbe aliyetakiwa kuthibitisha kauli au maelezo yake aliyoyatoa katika Bunge Maalum atashindwa kufanya hivyo, anaweza kujirekebisha kwa kufuta kauli au maelezo yake papo hapo au katika muda atakaokuwa amepewa na Mwenyekiti kwa ajili ya kuthibitisha kauli au usemi au maelezo yake.

(9) Endapo hadi kufikia mwisho wa muda aliopewa, Mjumbe aliyetakiwa kutoa uthibitisho wa ukweli wa kauli au maelezo yake aliyoyatoa Bungeni atakataa au atashindwa kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge Maalum na kama atakataa kujirekebisha kwa kufuta kauli au maelezo yake, basi Mwenyekiti atamwadhibu kwa kumsimamisha Mjumbe huyo asihudhurie vikao vya Bunge Maalum visivyoziid vitatu.

Muda wa
kusema
ndani ya
Bunge
Maalum

39. Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo kwenye Kanuni hizi au Mwenyekiti ameelekeza vinginevyo:-

- (a) Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba atakapokuwa anawasilisha Rasimu ya Katiba katika Bunge Maalum atasema kwa muda ambao Mwenyekiti wa Bunge Maalum ataona unafaa kwa ajili hiyo;
- (b) Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Maalum anayewasilisha hoja na maoni ya Kamati atawasilisha kwa muda usiozidi dakika thelathini.
- (c) kila Mjumbe anayejadili hoja, ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika kumi.

Kusema
zaidi ya
mara moja

40.(1) Isipokuwa tu kwa idhini ya Mwenyekiti, Mjumbe yeyote hataruhusiwa kusema zaidi ya mara moja kuhusu hoja, ila tu kama:-

- (a) anumia haki yake ya kujibu;
- (b) anasema kuhusu utaratibu; au
- (c) anasema kuomba kupata ufafanuzi wa jambo mahsusi linalohusu hoja inayojadiliwa ndani ya Bunge Maalum.

(2) Mjumbe ambaye amezungumza kuhusu hoja anaweza kuzungumza tena kuhusu hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja aliyoisemea.

(3) Wakati wa kujibu, mtoa hoja atapaswa kujibu mambo yale tu yaliyozungumzwa na Wajumbe waliochangia hoja yake na hataruhusiwa kutoa maelezo yoyote mapya, isipokuwa kama maelezo hayo ni ya lazima kwa madhumuni ya kufafanua jambo lililochangiwa na Wajumbe.

(4) Mjumbe yeyote hataruhusiwa kusema ndani ya Bunge Maalum kuhusu jambo baada ya Mwenyekiti kuwahoji Wajumbe na kura ya uamuzi ya aina yoyote kupigwa kuhusu jambo hilo.

Staha
ndani ya
Bunge

41.(1) Wakati wa Vikao vya Bunge Maalum, Mwenyekiti anapokuwa anaingia au kutoka katika Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum, Wajumbe na wageni wote waliopo kwenye Ukumbi huo watasimama kwa utulivu mahali pao na kubaki kimya hadi Mwenyekiti atakapokuwa ameketi katika Kiti chake au atakapokuwa ametoka kwenye Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum.

(2) Mjumbe aliyepo Bungeni wakati wa mjadala atatakiwa:

- (a) kuingia au kutoka kwenye Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum kwa staha na atainamisha kichwa kuelekeza kwa Mwenyekiti kwa heshima kila mara Mjumbe huyo atakapokuwa akienda au kutoka mahali pake;
- (b) kutulia na kukaa kwa heshima mahali pake, na hatatangatanga kwenye Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum;
- (c) kutopita kati ya kiti cha Mwenyekiti wa Bunge Maalum na Mjumbe anayesema;
- (d) kutosoma kitabu chochote, gazeti au barua, isipokuwa nyaraka zinazohusu shughuli za mjadala unaoendelea wakati huo.

(3) Mtumishi wa Bunge Maalum na mgeni yeyote aliyepo kwenye Ukumbi wa Mikutano ya Bunge na kwenye baraza za Ukumbi huo wakati wa mjadala atatakiwa:

- (a) kuingia au kutoka kwenye Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum kwa staha na atainamisha kichwa kuelekeza kwa Mwenyekiti kwa heshima, kila mara anapotoka au anapokwenda kukaa mahali pake;
- (b) kutulia na kukaa kwa heshima mahali pake, na hatatangatanga kwenye Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum;
- (c) kutosoma kitabu chochote, gazeti au barua, isipokuwa nyaraka zinazohusu shughuli za mjadala wa Bunge Maalum unaoendelea wakati huo.

Mamlaka ya
Mwenyekiti
kukatiza
majadiliano

42.(1) Mwenyekiti anaweza kulihutubia Bunge Maalum wakati wowote na kwa ajili hiyo, anaweza kumkatiza Mjumbe yeyote anayezungumza.

(2) Endapo Mwenyekiti atasimama wakati wa mjadala, na kuanza kuzungumza, Mjumbe yeyote ambaye atakuwa anazungumza wakati huo au ambaye atakuwa amesimama mahali pake akisubiri kuanza kuzungumza, ataketi mahali pake, na Bunge Maalum litabaki kimya ili Mwenyekiti aweze kutoa maelekezo au taarifa yake.

Haki ya
kuomba na
kupata
ufafanuzi

43.(1) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria na Kanuni hizi, Mjumbe yeyote atakuwa na haki ya kuomba na kupata ufafanuzi wa jambo lolote mahsusi linalohusu hoja inayojadiliwa ndani ya Bunge Maalum.

(2) Katika kutumia haki ya kuomba na kupata ufafanuzi kwa mujibu wa masharti ya fasili ya (1), Mjumbe analazimika kufuata utaratibu wa jinsi ya kupata nafasi ya kuitumia haki hiyo uliowekwa na Kanuni hizi, na muda wa kusema utakuwa ni dakika mbili.

(3) Haki ya Mjumbe kuomba na kupata ufafanuzi kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hii itapewa kipaumbele cha kwanza dhidi ya haki ya Mjumbe ya kusema Bungeni.

(4) Mjumbe yeyote anayekusudia kuomba na kupata ufafanuzi kwa mujibu wa Kanuni hii, atasimama mahala pake na kusema “*kuhusu ufafanuzi*”, akielekeza maneno hayo kwa Mwenyekiti.

(5) Baada ya kuitwa na Mwenyekiti kwa jina na kuruhusiwa kusema, Mjumbe aliyesimama kwa ajili ya kuomba na kupata ufafanuzi ataeleza kwa kifupi jambo hilo mahsusi analoliombea ufafanuzi, na wakati wa kusema ataelekeza maneno yake kwa Mwenyekiti.

(6) Baada ya kuhitimisha maelezo yake, Mjumbe mhusika ataketi mahali pake, na kama kuna Mjumbe mwingine aliyesimama kwa ajili ya kuomba na kupata ufafanuzi wa jambo lingine, Mwenyekiti atamwita jina na kumruhusu kusema; na kama hakuna Mjumbe mwingine, Mwenyekiti atatoa ufafanuzi ulioombwa na Mjumbe kabla ya kuruhusu mjadala wa hoja kuendelea

(7) Endapo Wajumbe wawili au zaidi watasimama wakati mmoja kuhusu jambo la ufafanuzi, Mwenyekiti atamwita Mjumbe atakayekuwa amemwona kwanza, na atafuatiwa na yule mwingine; na iwapo idadi ya Wajumbe waliosimama itakuwa ni zaidi ya wawili, basi Mwenyekiti atawaita kwa mpangilio atakaouona unafaa.

(8) Bila ya kuathiri masharti yaliyotangulia ya Kanuni hii, jambo lolote la ufafanuzi litashughulikiwa kwanza na Mwenyekiti kabla ya kuruhusu mjadala wa hoja inayohusiana na jambo linaloombewa ufafanuzi kuendelea.

Taarifa
kuhusu
utaratibu na
Mwongozo
wa
Mwenyekiti

44.(1) Mjumbe yeyote atakuwa na haki ya kuhoji kuhusu jambo lolote la utaratibu katika Bunge.

(2) Mjumbe anayetaka kuhoji kuhusu jambo la utaratibu anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno “*kuhusu utaratibu*”, ambapo Mjumbe yeyote ambaye wakati huo atakuwa anasema atanyamaza na kukaa chini na Mwenyekiti atamtaka Mjumbe aliyedai utaratibu ataje Kanuni au sehemu ya Kanuni iliyokiukwa.

(3) Mjumbe aliyedai utaratibu atalazimika kutaja Kanuni au sehemu ya Kanuni ya Bunge iliyokiukwa na muda wa kusema hautazidi **dakika moja**.

(4) Baada ya kutaja Kanuni au sehemu ya Kanuni iliyokiukwa, Mjumbe aliyesimama kuhusu utaratibu, ataketi mahali pake kusubiri uamuzi wa Mwenyekiti kuhusu suala hilo la utaratibu.

(5) Mwenyekiti anaweza, ama papo hapo kutoa uamuzi wake kuhusu jambo la utaratibu lililotajwa au kuahirisha uamuzi ili alifikirie zaidi jambo

hilo na kutoa uamuzi baadaye au kutoa uamuzi, baadaye kutoa sababu za uamuzi huo, vyovyote atakavyoona inafaa.

(6) Katika kufikia uamuzi, Mwenyekiti anaweza kuitaka Kamati ya Kanuni na Haki za Bunge Maalum au Kamati nyingine yoyote ya Bunge Maalum impe ushauri kuhusu jambo husika.

(7) Mjumbe aliyekuwa anazungumza wakati jambo la utaratibu lilipohojiwa anaweza kuendelea na hotuba yake baada ya Mwenyekiti kutoa uamuzi juu ya jambo hilo au baada ya kuahirisha uamuzi juu ya jambo hilo.

(8) Hali kadhalika, Mjumbe anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mjumbe mwingine anayesema na kuomba “*Mwongozo wa Mwenyekiti*” kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Mwenyekiti atoe ufafanuzi kama jambo hili linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge Maalum na majibu ya Mwenyekiti yatatolewa papo hapo au baadaye, kadri atakavyoona inafaa.

(9) Uamuzi wa Mwenyekiti kuhusu suala lolote la utaratibu katika Bunge Maalum utakuwa ni wa mwisho.

Hoja ya
kuahirisha au
kusitisha
mjadala

45.(1) Mjumbe yeyote anaweza kutoa hoja kwamba mjadala unaoendelea Bungeni uahirishwe au usitishwe hadi wakati wa baadae.

(2) Mjumbe anayependa mjadala unaoendelea kuhusu hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye, anaweza kutoa hoja “*Kwamba mjadala sasa uahirishwe*” na atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani, na pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala uahirishwe.

(3) Kama Mwenyekiti atakuwa na maoni kwamba kuwasilishwa kwa hoja hiyo ni kinyume cha uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge, atakataa kutoa ili iamuliwe; vinginevyo, papo hapo atawahoji Wajumbe kuhusu hoja hiyo kadri atakavyoona inafaa.

(4) Endapo hoja iliyowasilishwa haitapata kibali cha Bunge, mjadala kuhusu hoja iliyoko mbele ya Bunge utaendelea.

(5) Mjumbe yeyote hataruhusiwa kutoa hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja iliyotolewa kwa mujibu wa Kanuni hii.

Hoja ya
kufunga
mjadala

46.(1) Bila ya kuathiri masharti mengine ya Kanuni hii, Mjumbe yeyote anaweza kutoa hoja ya kufunga mjadala.

(2) Utaratibu utakaotumika ni kutoa hoja ya kufunga mjadala wakati ambapo bado kuna Wajumbe wanaopenda kuzungumza juu ya jambo lililoko katika mjadala, lakini muda uliotengwa umekwisha, au pale ambapo Bunge limewekewa kiwango cha juu cha muda wa kujadili hoja inayohusika na muda huo bado haujaisha.

(3) Hoja ya kufunga mjadala inaweza kutolewa baada ya hotuba yoyote kukamilika au ikiwa Mwenyekiti wa Bunge Maalum ataruhusu hoja ya kufanya mjadala mara tu au muda mfupi baada ya hoja hiyo kutolewa ili iamuliwe.

(4) Mjumbe anayetoa hoja ya kufunga mjadala, anaweza kusimama mahali pake na kutoa hoja “*Kwamba mjadala unaondelea sasa ufungwe*”.

(5) Endapo Mwenyekiti ataona kuwa hoja ya kufunga mjadala inakiuka mwenendo bora wa Shughuli za Bunge Maalum au inavunja haki za Wajumbe wa Bunge Maalum, basi ataikataa.

(6) Iwapo hoja “*Kwamba mjadala unaoendelea ufungwe*” itakubaliwa, basi Mwenyekiti atawahoji Wajumbe ili kuamua hoja hiyo.

Vikao vya
faragha vya
Bunge
Maalum

47.(1) Kwa kuzingatia hali na mazingira ya mjadala unavyoendelea ndani ya Bunge Maalum, Mwenyekiti wa Bunge Maalum anaweza kuamua mjadala husika uendeshwe katika kikao cha faragha cha Bunge Maalum.

(2) Hakuna mtu yeyote asiyekuwa Mjumbe au mtumishi wa Bunge Maalum atakayeruhusiwa kuwepo katika sehemu yoyote ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum wakati kikao cha faragha cha Bunge Maalum kikiendelea, isipokuwa watu maalum watakaokuwa wameruhusiwa na Mwenyekiti wa Bunge Maalum.

(3) Utaratibu utakaotumika katika kuendesha mjadala kwenye kikao cha faragha cha Bunge Maalum utaamuliwa na Mwenyekiti wa Bunge Maalum.

(4) Mwenyekiti wa Bunge Maalum anaweza kutoa taarifa fupi kwa wananchi kupitia vyombo vya habari, kuhusu majadiliano na uamuzi uliofanywa na Bunge Maalum katika kikao chake cha faragha, kama atakavyoona inafaa.

(5) Endapo Bunge Maalum litaona kwamba inafaa taarifa za mwenendo wa majadiliano katika kikao cha faragha zitolewe hadharani, Mwenyekiti wa Bunge Maalum ataagiza taarifa hizo zichapishwe katika taarifa rasmi za Bunge Maalum.

SEHEMU YA SITA

KAMATI ZA BUNGE MAALUM

Kamati za
Bunge
Maalum

48.(1) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria na Kanuni hizi, Bunge linaweza kuunda Kamati za Bunge Maalum za namna mbalimbali, kwa kadri litakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi na mamlaka yake.

(2) Bila ya kujali masharti ya fasili ya (1), kutakuwa na Kamati za Bunge Maalum zifuatazo:-

- (a) Kamati ya Shughuli za Bunge Maalum;
- (b) Kamati ya Kanuni na Haki za Bunge Maalum;
- (c) Kamati ya Uandishi;
- (d) Kamati Namba Moja;
- (e) Kamati Namba Mbili;;
- (f) Kamati Namba Tatu;
- (g) Kamati Namba Nne;
- (h) Kamati Namba Tano;
- (i) Kamati Namba Sita;
- (j) Kamati Namba Saba;
- (k) Kamati Namba Nane;
- (l) Kamati Namba Tisa;
- (m) Kamati Namba Kumi;
- (n) Kamati Namba Kumi na Moja;
- (o) Kamati Namba Kumi na Mbili;
- (p) Kamati Namba Kumi na Tatu;
- (q) Kamati Namba Kumi na Nne;
- (r) Kamati Namba Kumi na Tano;
- (s) Kamati Namba Kumi na Sita;
- (t) Kamati Namba Kumi na Saba.

(3) Majukumu ya Kamati za Bunge Maalum zilizoundwa kwa mujibu wa masharti ya fasili ya (2) yatakuwa kama yalivyoainishwa katika Kanuni hizi.

Muundo wa
Kamati za
Bunge
Maalum

49.(1) Kamati za Bunge Maalum zitaundwa na Mwenyekiti wa Bunge Maalum kwa namna ambayo itawezesha kila Mjumbe wa Bunge Maalum kuteuliwa kuwa mjumbe wa Kamati mojawapo.

(2) Wakati wa kufanya uteuzi wa mjumbe kuwa Mjumbe wa Kamati yoyote ya Bunge Maalum, Mwenyekiti wa Bunge Maalum atazingatia yafuatayo:

(a) kwa kadri inavyowezekana, idadi ya wajumbe inalingana kwa kila Kamati.

(b) uteuzi wa wajumbe katika kila Kamati utazingatia-

(i) uwiano wa Wajumbe wa Bunge Maalum kutoka pande zote za Muungano; na

(ii) idadi ya kila aina ya Wajumbe wa Bunge Maalum ilivyo katika Bunge Maalum.

(3) Katibu wa Bunge Maalum tahakikisha kuwa Wajumbe wote wa Bunge Maalum wanapewa orodha inayoonesha jinsi walivyopangwa katika Kamati mbalimbali.

(4) Ujumbe katika Kamati za Bunge Maalum utadumu kwa kipindi chote cha uhai wa Bunge Maalum.

(5) Bila ya kuathiri masharti mengine ya Kanuni hizi, wajumbe wa kila Kamati ya Bunge Maalum watamchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati kutoka miongoni mwao, ambao kwa muda wote wataokuwa Wajumbe, wataendelea kushika nafasi hizo kwa kipindi chote cha uhai wa Bunge Maalum.

(6) Kutakuwa na Sekretarieti ya kila Kamati ya Bunge Maalum itakayoundwa na watumishi kutoka katika Sekretarieti ya Bunge Maalum.

(7) Sekretarieti ya kila Kamati ya Bunge Maalum itakuwa na Wataalam wa masuala ya kibunge, Sheria, uandishi wa Sheria, utafiti na fani zingine za utaalam kwa ajili ya kuiwezesha Kamati kutekeleza ipasavyo majukumu yake, na itafanya kazi zake chini ya usimamizi wa Katibu wa Bunge Maalum.

(8) Bila ya kuathiri masharti ya fasili zilizotangulia za Kanuni hii, Katibu wa Bunge Maalum atateua mtumishi yeyote wa Sekretarieti ya Bunge Maalum kuwa Katibu wa Kamati ya Bunge Maalum, kwa ajili ya kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Kamati; na

(b) kuratibu shughuli za Kamati.

(9) Kwa ajili ya kutekeleza wajibu wake wa usimamizi kwa mujibu wa fasili ya (7), Katibu wa Bunge Maalum atakuwa na haki ya kuingia katika kikao chochote cha Kamati au Kamati Ndogo yoyote ya Kamati ya Bunge Maalum na kutoa maelekezo au ushauri kwa Katibu wa Kamati au mtumishi yeyote wa Sekretarieti ya Kamati husika ya Bunge Maalum kuhusu utaratibu unaotakiwa kufuatwa katika uendeshaji wa kikao kinachohusika cha Kamati.

Utaratibu wa
mikutano,
vikao na
akidi katika
Kamati za
Bunge

50.(1) Masharti ya Kanuni hii yanayoweka utaratibu wa kuendesha Mikutano, vikao na shughuli za Kamati yatatumika kwa Kamati zote za Bunge Maalum.

(2) Mwenyekiti wa Kamati ataongoza vikao vyote vya Kamati ya Bunge Maalum na endapo hayupo kwenye kikao, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ataongoza shughuli za kikao hicho, na ikiwa Mwenyekiti na Makamu wote hawapo, wajumbe waliohudhuria watamchagua mmojawapo miongoni mwao kuongoza kikao hicho.

(3) Kamati ya Bunge Maalum itakutana kila itakapoagizwa kukutana na Mwenyekiti wa Bunge Maalum au Mwenyekiti wa Kamati baada ya kupata idhini ya Mwenyekiti wa Bunge Maalum.

(4) Vikao vya kawaida vya Kamati za Bunge Maalum vitafanyika katika maeneo ya Bunge au katika maeneo mengine yaliyo nje ya maeneo ya Bunge Maalum yaliyoandaliwa kwa ajili hiyo.

(5) Kila Kamati ya Bunge Maalum itafanya vikao vyake kwa kuzingatia ratiba ya Shughuli za Bunge Maalum iliyowekwa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(6) Akidi ya vikao vyote vya Kamati ya Bunge Maalum itakuwa nusu ya wajumbe wote wa Kamati.

(7) Mambo yote yatakayojadiliwa na Kamati ya Bunge Maalum yataamuliwa kwa theluthi mbili ya wajumbe wa Kamati waliohudhuria na kupiga kura.

(8) Bila ya kuathiri masharti yaliyotangulia ya Kanuni hii, kila Kamati ya Bunge Maalum itajiwekea utaratibu wake, na inaweza kuwaruhusu Wajumbe ambao si wajumbe wa Kamati au watu ambao si wajumbe kuhudhuria na kushiriki katika shughuli za Kamati, lakini hawatakuwa na haki ya kupiga kura.

(9) Shughuli za kawaida za Kamati ya Bunge Maalum zitaendeshwa kwa uwazi ambapo Kamati kama itaona inafaa, inaweza kumwalika mtaalam yeyote ili kupata maoni na ushauri kwa ajili ya kuboresha jambo ambalo litakuwa linajadiliwa na Kamati hiyo.

(10) Mtu yeyote atakayealikwa kutoa maoni na ushauri wa jambo lolote kwenye Kamati ya Bunge Maalum kwa mujibu wa fasili ya (9)-

(a) atastahili haki na kinga zilizowekwa na Sheria na Kanuni hizi kuhusiana na maoni na ushauri atakaoutoa kwenye Kamati ya Bunge Maalum;

(b) atavaa vazi la heshima na pia atapaswa kuwa na nidhamu na kutii maelekezo ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Maalum.

(11) Bila ya kujali masharti ya fasili ya (9) ya Kanuni hii, shughuli zote za Kamati ya Bunge Maalum zinazohusu kuandaa na kutoa mapendekezo ya kuwasilishwa katika Bunge Maalum zitafanywa kwa faragha.

(12) Mwenyekiti wa Kamati yoyote ya Bunge Maalum atakuwa na mamlaka ya kuhakikisha kuwepo kwa amani na usalama, na pia nidhamu inayohitajika kwa ajili ya uendeshaji bora wa kazi na shughuli za Kamati; na kwa ajili hiyo, Mwenyekiti huyo anaweza kuchukua hatua za kinidhamu atakazooona zinafaa dhidi ya mjumbe yeyote wa Kamati atakayevuruga au atakayejaribu kuvuruga mwenendo bora wa kazi na shughuli za Kamati.

Vikao vya
faragha vya
Kamati za
Bunge
Maalum

51.(1) Kwa kuzingatia hali na mazingira ya mjadala unavyoendelea katika kikao cha Kamati, Mwenyekiti wa Kamati yoyote ya Bunge Maalum anaweza kuamua mjadala husika uendeshwe katika kikao cha faragha cha Kamati.

(2) Hakuna mtu yeyote asiyekuwa mjumbe wa Kamati au mtumishi wa Sekretareti ya Kamati atakayeruhusiwa kukaa katika sehemu yoyote ya Ukumbi wa mikutano ya Kamati wakati kikao cha faragha cha Kamati kinaendelea, isipokuwa watu maalum watakaokuwa wameruhusiwa na Mwenyekiti wa Kamati.

(3) Utaratibu utakaotumika katika kuendesha mjadala kwenye kikao cha faragha cha Kamati ya Bunge Maalum utaamuliwa na Mwenyekiti wa Kamati.

Muundo na
majukumu
ya Kamati ya
shughuli za
Bunge
Maalum

52.(1) Kutakuwa na Kamati ya Shughuli za Bunge Maalum ambayo itakuwa na Wajumbe wafuatao:-

- (a) Mwenyekiti wa Bunge Maalum ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;
- (b) Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati;
- (c) Wenyeviti wa Kamati za Bunge Maalum; na
- (d) Katibu atakuwa Katibu wa Kamati.

(2) Majukumu ya Kamati ya Shughuli za Bunge Maalum yatakuwa kama ifuatavyo:

- (a) kujadili na kuamua kuhusu mambo yote yanayohusu uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge Maalum na Kamati zake;

- (b) kujadili na kupanga ratiba ya utekelezaji wa Shughuli za Bunge Maalum; na
- (c) kujadili na kufanya uamuzi kuhusu masuala yatakayohitaji usuluhishi na maridhiano.

Majukumu
ya Kamati
ya Kanuni
na
Haki za
Bunge
Maalum

53.(1) Kutakuwa na Kamati ya Kanuni na Haki za Bunge Maalum itakayotekeleza majukumu yafuatayo:-

- (a) kujadili mapendekezo ya kuzifanyia marekebisho au mabadiliko Kanuni za Bunge Maalum yaliyopelekwa kwenye Kamati hiyo na Mwenyekiti wa Bunge Maalum, na kutoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Bunge Maalum;
- (b) kujadili na kutoa taarifa ya ufafanuzi, mwongozo au utaratibu kwa Mwenyekiti wa Bunge Maalum kuhusu jambo lolote la kikanuni litakalopelekwa kwenye Kamati hiyo na Mwenyekiti wa Bunge Maalum;
- (c) kuchunguza kuhusu masuala yote ya haki, kinga na madaraka ya Bunge Maalum yatakayopelekwa kwenye Kamati hiyo na Mwenyekiti wa Bunge Maalum, na kutoa mapendekezo na ushauri kwa Mwenyekiti wa Bunge Maalum kuhusu hatua zinazofaa kuchukuliwa;
- (d) kujadili na kumshauri Mwenyekiti wa Bunge Maalum kuhusu utekelezaji bora wa haki, kinga na madaraka ya Bunge Maalum; na
- (e) kushughulikia suala lolote linalohusiana na nidhamu ya Mjumbe yeyote wa Bunge Maalum lililopelekwa kwenye Kamati hiyo na Mwenyekiti wa Bunge Maalum.

(2) Bila ya kujali masharti ya Kanuni hii, wajumbe wa Kamati hii wanaweza kuteuliwa kuwa wajumbe wa Kamati nyingine zilizoundwa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati ya
Uandishi

54.(1) Kutakuwa na Kamati ya Uandishi itakayotekeleza majukumu yafuatayo:-

- (a) kuandaa Rasimu ya Katiba, kama ilivyopitishwa na Bunge Maalum kutokana na uamuzi wa Bunge Maalum kuhusu taarifa za Kamati Namba Moja hadi Namba Kumi na Saba za Bunge Maalum; na
- (c) kuwasilisha mbele ya Bunge Maalum, Rasimu ya Katiba iliyotajwa katika aya ya (a) ili ipigiwe kura ya mwisho na kupitishwa na Bunge Maalum kwa ujumla wake.

Majukumu
ya Kamati
Kamati
Namba
Moja

55. Majukumu ya Kamati Namba Moja yatakuwa ni:-

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;
- (b) kujadili na kuwasilisha mbele ya Bunge Maalum, taarifa kuhusu mambo yaliyomo katika Sura ya Kwanza ya Rasimu ya Katiba kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati
Namba
Mbili

56. Majukumu ya Kamati Namba Mbili yatakuwa ni:-

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;
- (b) kujadili mambo yote yaliyomo katika Sura ya Pili ya Rasimu ya Katiba na kutoa taarifa kwenye Bunge Maalum kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati
Namba
Tatu

57. Majukumu ya Kamati Namba Tatu yatakuwa ni:-

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;
- (b) kujadili mambo yote yaliyomo katika Sura ya Tatu ya Rasimu ya Katiba na kutoa Taarifa Bungeni kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati
Namba Nne

58. Majukumu ya Kamati Namba Nne yatakuwa ni:-

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;
- (b) kujadili mambo yote yaliyomo katika Sura ya Nne ya Rasimu ya Katiba na kutoa Taarifa Bungeni kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati
Namba Tano

59. Majukumu ya Kamati Namba Tano yatakuwa ni:

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;
- (b) kujadili mambo yote yaliyomo katika Sura ya Tano ya Rasimu ya Katiba na kutoa Taarifa Bungeni kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati
Namba Sita

60. Majukumu ya Kamati Namba Sita yatakuwa ni:-

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;
- (b) kujadili mambo yote yaliyomo katika Sura ya Sita ya Rasimu ya Katiba na kutoa Taarifa Bungeni kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati
Namba
Saba

61. Majukumu ya Kamati Namba Saba yatakuwa ni:-

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;
- (b) kujadili mambo yote yaliyomo katika Sura ya Saba ya Rasimu ya Katiba na kutoa Taarifa Bungeni kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati
Namba
Nane

62. Majukumu ya Kamati Namba Nane yatakuwa ni:-

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;
- (b) kujadili mambo yote yaliyomo katika Sura ya Nane ya Rasimu ya Katiba na kutoa Taarifa Bungeni kwa mujibu wa

masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati
Namba Tisa

63. Majukumu ya Kamati Namba Tisa yatakuwa ni:-

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;
- (b) kujadili na kuwasilisha mbele ya Bunge Maalum, taarifa kuhusu mambo yaliyomo katika Sura ya Tisa ya Rasimu ya Katiba kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati
Namba
Kumi

64. Majukumu ya Kamati Namba Kumi yatakuwa ni:-

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;
- (b) kujadili na kuwasilisha mbele ya Bunge Maalum, taarifa kuhusu mambo yaliyomo katika Sura ya Kumi ya Rasimu ya Katiba kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati
Namba
Kumi na
Moja

65. Majukumu ya Kamati Namba Kumi na Moja yatakuwa ni:-

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika Sura zote za Rasimu kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;
- (b) kujadili na kuwasilisha mbele ya Bunge Maalum, taarifa kuhusu mambo yaliyomo katika Sura ya Kumi na Moja ya Rasimu ya Katiba kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati
Namba
Kumi na
Mbili

66. Majukumu ya Kamati Namba Kumi na Mbili yatakuwa ni:-

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;

- (b) kujadili na kuwasilisha mbele ya Bunge Maalum, taarifa kuhusu mambo yaliyomo katika Sura ya Kumi na Mbili ya Rasimu ya Katiba kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati
Namba
Kumi na
Tatu

67. Majukumu ya Kamati Namba Kumi na Tatu yatakuwa ni:-

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;
- (b) kujadili na kuwasilisha mbele ya Bunge Maalum, taarifa kuhusu mambo yaliyomo katika Sura ya Kumi na Tatu ya Rasimu ya Katiba kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati
Namba
Kumi na
Nne

68. Majukumu ya Kamati Namba Kumi na Nne yatakuwa ni:-

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;
- (b) kujadili na kuwasilisha mbele ya Bunge Maalum, taarifa kuhusu mambo yaliyomo katika Sura ya Kumi na Nne ya Rasimu ya Katiba kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati
Namba
Kumi na
Tano

69. Majukumu ya Kamati Namba Kumi na Tano yatakuwa ni:-

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;
- (b) kujadili na kuwasilisha mbele ya Bunge Maalum, taarifa kuhusu mambo yaliyomo katika Sura ya Kumi na Tano ya Rasimu ya Katiba kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati
Namba
Kumi na
Sita

70. Majukumu ya Kamati Namba Kumi na Sita yatakuwa ni:-

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;

- (b) kujadili na kuwasilisha mbele ya Bunge Maalum, taarifa kuhusu mambo yaliyomo katika Sura ya Kumi na Tatu ya Rasimu ya Katiba kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Majukumu
ya Kamati
Namba
Kumi na
Saba

71. Majukumu ya Kamati Namba Kumi na Saba yatakuwa ni:-

- (a) kujadili mambo yote yaliyomo katika Sura zote za Rasimu na kujadili mambo yote yaliyomo katika sura zote za Rasimu ya Katiba na endapo linahitaji kuzingatiwa na Kamati nyingine ya Bunge Maalum, basi italiwasilisha jambo hilo kwenye Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kwa ajili ya kuzingatiwa;

- (b) kujadili na kuwasilisha mbele ya Bunge Maalum, taarifa kuhusu mambo yaliyomo katika Sura ya Kumi na Tatu ya Rasimu ya Katiba kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Upangaji wa
ratiba ya
utekelezaji
wa kazi na
majukumu
ya Bunge
Maalum
Sura 83

72.(1) Katika kipindi cha siku saba baada ya Kanuni hizi kupitishwa, Bunge Maalum kupitia Kamati ya Shughuli za Bunge Maalum itaandaa ratiba ya utekelezaji wa kazi na majukumu ya Bunge Maalum na Kamati zake, kwa kuzingatia muda uliowekwa na Sheria.

(2) Ratiba ya utekelezaji wa kazi na majukumu ya Bunge Maalum iliyoandaliwa kwa mujibu wa fasili ya (1) ambayo itaitwa “ratiba ya Shughuli” itatekelezwa kama sehemu ya Kanuni hizi.

(3) Endapo itatokea haja ya kuifanyia marekebisho, pendekezo la kuifanyia marekebisho ratiba hiyo ya shughuli litajadiliwa na kufanyiwa uamuzi na Kamati ya Shughuli ya Bunge Maalum.

Kazi za
Kamati na
utekelezaji
wake

73.(1) Kabla ya kuanza kutekeleza kazi na majukumu yake yaliyowekwa kwa mujibu wa Kanuni hizi, kila Kamati ya Bunge Maalum itaandaa orodha ya kazi na majukumu yanayotakiwa kutekelezwa na Kamati husika, pamoja na ratiba kwa ajili ya utekelezaji wa kazi na majukumu hayo.

(2) Orodha ya kazi na majukumu ya kila Kamati ya Bunge Maalum ikiambatana na ratiba ya utekelezaji wake iliyoandaliwa kwa mujibu wa fasili ya (1), vitawasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati husika katika kikao cha Kamati ya Shughuli ya Bunge Maalum kwa ajili ya kujadiliwa na kuzingatiwa katika ratiba ya Shughuli za Bunge Maalum itakayowekwa na Kamati ya Shughuli ya Bunge Maalum.

Utaratibu wa
kufanya
uamuzi
katika
Kamati za
Bunge

74.(1) Maoni ya Kamati ya Bunge Maalum yatakuwa ni yale yaliyokubaliwa na theluthi mbili ya wajumbe wa Kamati waliohudhuria na kupiga kura, na yatawasilishwa kwenye Bunge Maalum na Mwenyekiti wa Kamati au mjumbe mwingine wa Kamati ya Bunge Maalum.

(2) Mjumbe yeyote wa Kamati ya Bunge Maalum hataruhusiwa kuzungumzia hadharani maoni ya Kamati kuhusu jambo lolote litakalokuwa linashughulikiwa na Kamati kabla maoni hayo hayajawasilishwa rasmi kwenye Bunge Maalum.

(3) Kamati yoyote ya Bunge Maalum inaweza kuunda Kamati Ndogo kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli zake, kadri itakavyoona inafaa, na kila Kamati Ndogo itapangiwa kazi zake na Kamati ya Bunge Maalum inayohusika.

(4) Kila Kamati ya Bunge Maalum itakuwa na jukumu la kujadili maudhui ya Rasimu ya Katiba kuhusiana na mambo yaliyo chini ya mamlaka yake na kuandaa taarifa ya Kamati itakayowasilishwa katika Bunge Maalum kwa ajili ya kujadiliwa.

(5) Bila ya kujali iwapo umepangwa muda maalum au la kwa ajili ya Kamati ya Bunge Maalum kujadili maudhui ya Rasimu ya Katiba, Mwenyekiti wa Kamati anaweza kuufupisha mjadala huo endapo ataona unarefushwa bila sababu ya msingi wala tija yoyote.

(6) Baada ya kukamilisha kazi yake, itakuwa ni lazima kwa kila Kamati ya Bunge Maalum kuwasilisha kwenye Bunge Maalum taarifa ya mambo ililokuwa inayafanyia kazi, kwa madhumuni ya kujadiliwa na kupata uamuzi wa Bunge Maalum.

(7) Taarifa ya Kamati ya Bunge Maalum itakayowasilishwa kwenye Bunge Maalum kwa mujibu wa fasili (1), itawasilishwa kama hoja ya Kamati.

(8) Mwenyekiti wa Bunge Maalum ataweka utaratibu wa kujadili taarifa za Kamati za Bunge Maalum ambapo taarifa ya Kamati ya Bunge Maalum inapowasilishwa katika Bunge Maalum, itajadiliwa kwa kufuata mpangilio wa Shughuli za Bunge Maalum.

Wajibu wa
Mjumbe
kuhudhuria
vikao na
ukomo wa
Kamati

75.(1) Utakuwa ni wajibu wa kwanza kwa kila mjumbe wa Kamati ya Bunge Maalum kuhudhuria vikao vya Kamati kwa wakati uliopangwa.

(2) Mjumbe yeyote ambaye hatahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Kamati bila sababu zozote za msingi, atapewa onyo na Mwenyekiti wa Kamati, na endapo ataendelea mara mbili au zaidi kutohudhuria vikao vya Kamati baada ya kupewa onyo, Mwenyekiti wa Kamati atalipeleka jina lake kwa Mwenyekiti wa Bunge ili aliwasilishe katika Kamati ya Kanuni na Haki za Bunge Maalum kupata ushauri wa hatua za kinidhamu zinazofaa kuchukuliwa dhidi yake.

(3) Mjumbe ambaye jina lake litapelekwa kwenye Kamati ya Kanuni na Haki za Bunge kwa mujibu wa fasili ya (2) anaweza kupewa adhabu au

kuchukuliwa hatua yoyote ya kinidhamu itakayopendekezwa na Kamati hiyo.

(4) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa fasili ya (2), mjumbe yeyote wa Bunge Maalum mwenye udhuru, atalazimika kutoa taarifa ya maandishi kwa Mwenyekiti wa Bunge na nakala kwa Mwenyekiti wa Kamati na Katibu wa Bunge kuhusu kutohudhuria kwake, na taarifa hiyo itahifadhiwa na Kamati kwa ajili ya kumbukumbu.

(5) Kamati za Bunge Maalum zilizoundwa kwa mujibu wa Kanuni hizi zitakoma baada ya maisha ya Bunge Maalum kufikia ukomo wake.

SEHEMU YA SABA

UTARATIBU WA KUWASILISHA, KUJADILI NA KUPITISHA MASHARTI YA RASIMU YA KATIBA

Utaratibu wa kuwasilisha Rasimu ya Katiba sura ya 83

76.(1) Rasimu ya Katiba itawasilishwa katika Bunge Maalum na Mwenyekiti wa Tume, kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 20(3) cha Sheria.

(2) Hakutakuwa na majadala wowote utakaofanyika wakati wa Rasimu ya Katiba itakapowasilishwa kwenye Bunge Maalum.

(3) Baada ya Rasimu ya Katiba kuwasilishwa kwa mujibu wa fasili ya (1), Mwenyekiti wa Bunge Maalum atalihakikisha Bunge kwa muda atakaona unafaa kwa ajili ya kuwawezesha Wajumbe kupata muda wa kuisoma Rasimu ya Katiba.

(4) Bunge Maalum litakapokutana tena baada ya kuahirishwa kwa mujibu wa fasili ya (3), Mwenyekiti wa Bunge Maalum atatangaza majina ya wajumbe wa kila Kamati ya Bunge Maalum, na kila Kamati itatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

Rasimu ya Katiba kupelekwa kwenye Kamati

77.(1) Mwenyekiti atapeleka nakala za Rasimu ya Katiba katika Kamati za Bunge Maalum, na kila Kamati ya Bunge Maalum itajadili Rasimu hiyo kwa mujibu wa mgawanyo wa majukumu ya Kamati za Bunge Maalum uliowekwa na Kanuni hizi.

(2) Baada ya Kamati ya Bunge Maalum kukamilisha kazi ya kujadili Rasimu ya Katiba kwa mujibu wa masharti ya fasili ya (1), Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Maalum atamjulisha Mwenyekiti wa Bunge Maalum kwa maandishi kwamba, Kamati imemaliza kazi ya kujadili Sura ya Rasimu ya Katiba inayohusika nayo.

(3) Baada ya kupokea taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Maalum kwa mujibu wa fasili ya (2), Mwenyekiti wa Bunge ataagiza taarifa ya Kamati iwekwe kwenye Orodha ya Shughuli kwa ajili ya kuwasilishwa na

kujadiliwa katika Bunge Maalum kama hoja ya Kamati kwa mujibu wa ratiba ya shughuli, ili kupata Uamuzi wa Bunge Maalum.

Uwasilishaji
wa hoja ya
Kamati

78.(1) Isipokuwa kama Kamuni hizi zimeelekeza vinginevyo, hakuna mjadala wowote utakaoendeshwa Bungeni ila tu mjadala unaohusu shughuli iliyoingizwa kwenye Kitabu cha Orodha ya Shughuli za Bunge na kuwekwa kwenye Orodha ya Shughuli z akikao hicho.

(2) Hoja zote zitaingizwa kwenye Kitabu cha Shughuli za Bunge Maalum kitakachoandaliwa na Katibu, na zitawekwa kwenye Orodha ya Shughuli ya kikao cha Bunge Maalum kulingana na maelkezo ya Mwenyekiti.

(3) Siku ambayo taarifa ya Kamati kuhusu Sura ya Rasimu ya Katiba imepangwa katika Orodha ya Shughuli, Mwenyekiti wa Kamati husika ya Bunge Maalum husika au mjumbe wa Kamati hiyo aliyeteuliwa na Mwenyekiti wa Kamati kwa ajili hiyo, atawasilisha hoja kwamba, Taarifa ya Kamati hiyo Isomwe na kujadiliwa Bungeni.

(4) Hoja ikishawekwa kwenye Orodha ya Shughuli itawasilishwa na kuamuliwa Bungeni kwa utaratibu kwamba, baada ya Mwenyekiti wa Kamati iliyopelekewa hoja hiyo kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, Mwenyekiti wa Bunge ataelekeza hoja hiyo ijadiliwe.

(5) Hoja yoyote ya Kamati itakayowasilishwa katika Bunge Maalum kwa mujibu wa Kanuni hii itawekwa katika lugha ambayo italiwezesha Bunge kufanya uamuzi ambao ni bayana.

(6) Mwenyekiti wa Kamati husika ya Bunge Maalum au mjumbe mwingine wa Kamati hiyo aliyeteuliwa kwa ajili hiyo, atasoma kwa ufupi taarifa ya Kamati kuhusu Sura ya Rasimu ya Katiba na kutoa hoja kwamba taarifa hiyo ijadiliwe Bungeni.

(7) Hoja ya taarifa ya Kamati Kusomwa na kujadiliwa Bungeni itakuwa kama ifuatavyo:-

“Kwamba, taarifa ya Kamati Namba..... sasa isomwe na kujadiliwa na Bunge Maalum, naomba kutoa Hoja.”

(8) Baada ya hoja ya Kamati kutolewa katika Bunge Maalum na Mwenyekiti wa Bunge Maalum kuelekeza hoja hiyo ijadiliwe, mjadala kuhusu taarifa ya Kamati utaanza.

(9) Mwenyekiti wa Bunge Maalum kwa kushauriana na Kamati ya Shughuli, atapanga muda utakaotumika kujadili taarifa ya kila Kamati ya Bunge Maalum, kwa kuzingatia muda uliowekwa na Sheria, pamoja na ratiba ya shughuli iliyowekwa kwa mujibu wa Kanuni hizi, kwa ajili ya Bunge Maalum kutekeleza majukumu yake.

(10) Wakati wa mjadala huo, Mjumbe yeyote wa Bunge Maalum anaweza kushauri na kutoa mapendekezo ya marekebisho au mabadiliko kwa ajili ya kuboresha masharti yaliyomo katika Sura ya Rasimu ya Katiba inayohusika na taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni.

(11) Mwenyekiti wa Bunge Maalum hataruhusu hoja yoyote inayokiuka Sheria au masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi.

(12) Kila hoja itawekwa kwenye Orodha ya Shughuli ikiwa kama ilivyowasilishwa au kama ilivyofanyiwa marekebisho au mabadiliko.

Masharti
kuhusu
mapende-
kezo ya
Kamati

79.(1) Bila kujali masharti mengine yaliyowekwa na Kanuni hizi, Bunge Maalum halitashughulikia pendekezo lolote la Kamati ambalo linahusu jambo ambalo lipo nje ya mamlaka ya Bunge Maalum.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya fasili ya (1), mapendekezo yoyote ya marekebisho au mabadiliko hayatakubaliwa iwapo:

(a) yanapendekeza kufuta au kuondoa misingi mikuu ya kitaifa iliyowekwa na kifungu cha 9(2) cha Sheria; au

(b) yanakiuka au kwenda kinyume na uamuzi wa Bunge Maalum uliokwishaanyika awali.

Utaratibu wa
majadiliano
wakati wa
kujadili
taarifa ya
Kamati

80.(1) Kwa kuzingatia mamlaka ya Bunge Maalum ya kujadili na kupitisha Rasimu ya Katiba yaliyowekwa na Sheria, **msingi wa majadiliano** ya Bunge Maalum utakuwa ni **mapendekezo yatakayowasilishwa na Kamati ya Bunge Maalum inayohusika kupitia taarifa ya Kamati itakayowasilishwa katika Bunge Maalum kama hoja ya Kamati.**

(2) Mwenyekiti wa Bunge Maalum atakuwa na mamlaka ya kuamua kama pendekezo lolote la Kamati ya Bunge Maalum au la Mjumbe yeyote wa Bunge Maalum linakubalika au halikubaliki kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi, na **uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho.**

(3) Mjumbe wa Bunge Maalum baada ya kuitwa na Mwenyekiti wa Bunge Maalum kujadili hoja, atasimama mahali pake na kutoa maelezo yake, kuhusu hoja hiyo kwa kuyaelekeza kwa Mwenyekiti.

(4) Katika kujadili taarifa au hoja ya Kamati, kila Mjumbe wa Bunge Maalum atakayepata nafasi ataelekeza maelezo yake kwenye hoja au jambo mahsusi linalojadiliwa kwa wakati huo, na endapo Mjumbe yeyote ataanza kujadili au kutoa maelezo ambayo hayahusiani na hoja au jambo mahsusi linalojadiliwa kwa wakati huo au anarudiarudia maelezo yaliyokwishatolewa na Mjumbe au Wajumbe wengine, Mwenyekiti wa

Bunge Maalum atamwamuru Mjumbe huyo akatishe maelezo yake na kukaa chini.

(5) Mjumbe wa Bunge Maalum aliyeamriwa na Mwenyekiti wa Bunge Maalum kukatisha maelezo yake na kukaa chini kwa mujibu wa fasili ya (4) atatii amri ya Mwenyekiti bila ukaidi wowote, na iwapo atakaidi, ataadhibiwa na Mwenyekiti papo hapo, kwa mujibu wa mamlaka aliyonayo ya kusimamia Kanuni hizi na pia uendes haji bora wa Shughuli za Bunge Maalum.

(6) Endapo wakati mjadala unaendelea ndani ya Bunge Maalum na Mjumbe yeyote wa Bunge Maalum anahitaji kupata ufafanuzi wa jambo lolote linalojadiliwa, anaweza kuomba na kupata ufafanuzi huo kutoka kwa Mwenyekiti wa Bunge Maalum bila mjadala wowote, kwa mujibu wa utaratibu wa kuomba ufafanuzi uliowekwa na Kanuni hizi.

(7) Wakati wa kujadili taarifa au hoja ya Kamati ya Bunge Maalum, Mwenyekiti wa Kamati inayohusika au mjumbe mwingine wa Kamati hiyo ndiye atakayewajibika kutoa maelezo ya ufafanuzi na kujibu hoja mbalimbali zitakazotolewa na Wajumbe wa Bunge Maalum wakati wa mjadala.

(8) Endapo majibu au ufafanuzi kuhusu hoja zilizojitokeza wakati wa mjadala wa hoja ya Kamati ya Bunge Maalum hautatolewa kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge Maalum, Mwenyekiti wa Bunge Maalum ataliahirisha Bunge Maalum na kuelekeza Kamati husika ijadili na kupata majibu ya hoja zilizojitokeza, kabla ya kurejea tena kwenye Bunge Maalum kwa ajili ya kuwasilisha tena majibu ya hoja hizo katika siku na muda kama Mwenyekiti atakavyoelekeza.

Utaratibu wa kupiga kura kupitisha mapendekezo ya marekebisho

81.(1) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria na Kanuni hizi, mapendekezo ya marekebisho au mabadiliko yaliyokidhi matakwa na masharti ya Kanuni hizi yatajadiliwa na kupigiwa kura kwanza kabla ya Sura au Sehemu au Ibara inayohusika ya Rasimu ya Katiba kupigiwa kura na kupitishwa.

(2) Mapendekezo ya marekebisho au mabadiliko yaliyowasilishwa kwa mujibu wa fasili ya (1) yatajadiliwa na kupigiwa kura moja baada ya jingine, isipokuwa kwamba, pale ambapo marekebisho au mabadiliko hayo yanahusu jambo moja, Mwenyekiti anaweza kuelekeza yapigiwe kura kwa pamoja.

(3) Pale ambapo mapendekezo ya marekebisho au mabadiliko yatakubaliwa, basi Sura, Sehemu au Ibara inayohusika ya Rasimu ya Katiba itahesabiwa kuwa imepitishwa pamoja na mabadiliko yake:

Isipokuwa kwamba, pale ambapo mapendekezo ya marekebisho au mabadiliko yatakataliwa, Sura, Sehemu au Ibara inayohusika ya Rasimu ya Katiba itahesabiwa kuwa imepitishwa bila marekebisho au mabadiliko.

82.(1) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria na Kanuni hizi, utaratibu wa Bunge Maalum kufanya uamuzi utakuwa ni kwa Mwenyekiti kulihoji Bunge Maalum na kupata Uamuzi wa Bunge Maalum utakaotokana na wingi wa idadi ya Wajumbe kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi:

Isipokuwa kwamba, ili Rasimu ya Katiba iweze kupitishwa katika Bunge Maalum itahitaji kuungwa mkono kwa wingi wa theluthi mbili ya idadi ya Wajumbe kutoka Tanzania Zanzibar.

(2) Iapo jambo lolote linahitaji kuamuliwa au kutekelezwa na Bunge Maalum, basi jambo hilo halitahesabiwa kuwa limeamuliwa au limetekelezwa ipasavyo, ila mpaka liwe limeamuliwa au limetekelezwa na Bunge Maalum kwa kuzingatia masharti na utaratibu uliowekwa na Sheria pamoja na Kanuni hizi.

(3) Kwa madhumuni ya Kanuni hii, utaratibu utakaotumika kupata uamuzi baada ya Mwenyekiti wa Bunge Maalum kutoa swali la kulihoji Bunge Maalum utakuwa ni kwa:

(a) kura ya siri, au

(b) Kura ya kielektroniki.

(4) Mwenyekiti wa Bunge Maalum anaweza kutumia mojawapo ya utaratibu wa kura iliowekwa na masharti ya fasili ya (3) kwa kuzingatia jambo husika lilivyo, kwa kadri atakavyoona inafaa.

(5) Bila ya kujali masharti ya fasili ya (4), Mjumbe yeyote wa Bunge Maalum anaweza kutoa hoja kupendekeza mojawapo ya utaratibu wa kura uliowekwa na fasili ya (3) utumike, kwa kuzingaia mazingira ya jambo husika, na pia uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge Maalum.

(6) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria na Kanuni hizi, wakati wa kupata umauzi wa Bunge Maalum kuhusu kupitisha Rasimu ya Katiba, Bunge Maalum litapiga kura ya siri, ambayo kwa madhumuni ya Kanuni hii, itaitwa “kura ya mwisho”.

(7) Hoja iliyowasilishwa na Kamati ya Bunge Maalum katika Bunge Maalum itaamuliwa kwa kuungwa mkono kwa wingi wa idadi ya theluthi mbili ya Wajumbe wote wa Bunge Maalum kutoka Tanzania Bara na theluhi mbili ya idadi ya Wajumbe wote wa Bunge Maalum kutoka Tanzania Zanzibar.

(8) Wakati amekalia kiti cha Mwenyekiti wa Bunge Maalum, Mwenyekiti wa Bunge Maalum hatakuwa na kura ya kawaida bali atakuwa na kura ya uamuzi endapo kura ya “Ndiyo” na “Siyo” zitalinga.

83.(1) Wakati wa kupiga kura ya siri, kila Mjumbe atapiga kura ya “Ndiyo” au “Hapana”, kwa kutumia karatasi za kupigia kura zitakazokuwa zimeandaliwa na Katibu wa Bunge Maalum kwa ajili hiyo.

(2) Upigaji kura utakuwa ni kwa Mjumbe baada ya kupewa karatasi ya kupigia kura, kuweka alama ya ✓ kwenye moja ya kisanduku kilichopo sanjai na maneno “Ndiyo” na “Hapana”, kwa jinsi yeye binafsi anavyoona inafaa.

(3) Mjumbe ambaye kwa bahati mbaya ataharibu karatasi yake ya kupigia kura atairudisha karatasi hiyo iliyoharibika kwa Makatibu Wasaidizi na atapewa karatasi nyingine ya kupigia kura.

(4) Mjumbe ambaye atakuwa na mahitaji maalum au atakuwa anahitaji usaidizi katika zoezi la kupiga kura, atapatiwa mahitaji hayo na usaidizi huo kwa utaratibu ulioandaliwa na Sekretarieti ya Bunge Maalum kwa ajili hiyo.

(5) Baada ya kila Mjumbe aliyehudhuria kikao kupiga kura, kura hizo zitakusanywa na kuwekwa kwenye masanduku ya kura na kupelekwa kwenye chumba maalum kitakachokuwa kimeandaliwa kwa ajili ya kuhesabu kura.

(6) Baada ya kura kuhesabiwa, Katibu wa Bunge Maalum atatangaza matokeo ya kura, na matokeo hayo yataingizwa katika taarifa rasmi za Bunge Maalum.

Kura ya
kielektroniki

84.(1) Upigaji kura kwa elektroniki utatumika pale ambapo Mwenyekiti au Mjumbe yeyote atapendekeza, na Bunge kukubali kwamba utumike.

(2) Pale ambapo utaratibu huo wa upigaji kura umeamuliwa utumike, lakini kutokana na matatizo ya kiufundi utashindwa kutumika, basi upigaji wa kura utafanyika kwa utaratibu wa kura ya siri.

(3) Endapo utaratibu wa kura ya kielektroniki utatumika, basi kumbukumbu za matokeo ya kura hiyo zitahusu idadi ya kura za “Ndiyo” au “Hapana”, kwa tarakimu bila majina.

Utaratibu wa
kupiga kura
na kupitisha
masharti ya
Rasimu ya
Katiba

85.(1) Bila ya kuathiri masharti mengine ya Kanuni hizi, utaratibu utakaotumika kwa ajili ya Bunge Maalum kutumia mamlaka yake ya kujadili na kupitisha masharti ya Rasimu ya Katiba utakuwa kama ifuatavyo:-

- (a) kujadili na kupigia kura marekebisho au mabadiliko ya kuboresha Rasimu ya Katiba yaliyowasilishwa na Kamati za Bunge; na
- (b) kujadili na kupiga kura ya mwisho kwa ajili ya kupitisha Rasimu ya Katiba kwa ujumla wake.

(2) Endapo taarifa ya Kamati ya Bunge Maalum inayohusika haitapendekeza marekebisho yoyote ya kuboresha Rasimu ya Katiba, basi masharti ya Sura inayohusika ya Rasimu ya Katiba yatachukuliwa kwamba yamepitishwa kama yalivyo bila ya marekebisho au mabadiliko yoyote.

(3) Kupiga kura kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hii itakuwa ni wajibu na haki ya msingi ya kila Mjumbe wa Bunge Maalum, na kila Mjumbe atapiga kura kwa binafsi yake:

Isipokuwa kwamba, Mjumbe ambaye anahitaji usaidizi au nyenzo maalum kwa ajili ya kupiga kura mwenyewe, atapatiwa usaidizi au nyenzo hiyo kwa ajili ya kumwezesha kupiga kura.

Utaratibu wa
kupitisha
Rasimu ya
Katiba

86.(1) Baada ya Bunge Maalum kukamilisha shughuli ya kujadili na kupitisha mapendekezo ya Kamati zote za Bunge Maalum ya kuboresha Rasimu ya Katiba kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi, Mwenyekiti wa Bunge Maalum ataiagiza Kamati ya Uandishi ya Bunge Maalum kuandaa nakala ya Rasimu ya Katiba kama ilivyopitishwa na Bunge, wakati wa kupitisha mapendekezo hayo ya Kamati za Bunge Maalum.

(2) Baada ya Kamati ya Uandishi ya Bunge Maalum kukamilisha kazi yake kwa mujibu wa masharti ya fasili ya (1), Mwenyekiti wa Kamati hiyo atamwarifu kwa maandishi Mwenyekiti wa Bunge kuhusu kukamilika kwa kazi hiyo.

(3) Baada ya Mwenyekiti wa Bunge Maalum kupokea taarifa iliyowasilishwa kwa mujibu wa fasili ya (2), ataagiza Rasimu ya Katiba iliyoandaliwa kwa mujibu wa masharti ya fasili ya (1) iwekwe kwenye Orodha ya Shughuli kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye Bunge Maalum na kupitishwa kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 81(2).

Hoja ya
kuwasilisha
Rasimu ya
Katiba

87.(1) Hoja ya kuwasilisha Rasimu ya Katiba katika Bunge Maalum kwa mujibu wa fasili hii itakayowasilishwa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Uandishi ya Bunge Maalum itakuwa katika maneno yafuatayo:-

“Kwamba, Rasimu ya Katiba, kama ilivyopitishwa Sura kwa Sura na Bunge Maalum, sasa ijadiliwena kupitishwa kwa ujumla wake “

(2) Baada ya hoja ya kuwasilisha Rasimu ya Katiba kwa mujibu wa fasili ya (1) kutolewa, Bunge litaanza mjadala wa jumla kuhusu Rasimu hiyo, na katika hatua hii, mjadala utahusu ubora wa misingi na maudhui ya Rasimu hiyo tu; ambapo mjadala kuhusu Sehemu, Sura au ibara za Rasimu, wala mapendekezo ya marekebisho yoyote katika Rasimu hiyo hayatakubaliwa.

(3) Baada ya majadiliano wa jumla kwa mujibu wa fasili ya (2) kukamilika, Rasimu ya Katiba itapitishwa na Bunge Maalum kwa mujibu wa masharti ya Sheria pamoja na masharti ya Kanuni hizi.

(4) Baada ya kupitisha Rasimu ya Katiba kwa mujibu wa fasili ya (3), Bunge Maalum litapitisha Utangulizi na Jina la Rasimu ya Katiba.

Kufanya masahihisho ya kuondoa makosa ya uchapishaji katika Rasimu ya Katiba

88. Mwenyekiti anaweza kumuagiza Katibu wa Bunge Maalum kuifanyia masahihisho Rasimu ya Katiba iliyopitishwa na Bunge Maalum, kwa ajili ya kuondoa makosa ya uchapishaji, kabla ya saini za Wajumbe wa Bunge Maalum kuambatanishwa kwenye Rasimu hiyo.

Ridhaa ya Bunge Maalum na hifadhi ya Rasimu ya Katiba

89. (1) Rasimu ya Katiba kama ilivyopitishwa na Bunge Maalum, itaidhinishwa kwa kuwekwa saini na kila Mjumbe wa Bunge Maalum na kuthibitishwa na Katibu wa Bunge Maalum, na Mwenyekiti wa Bunge Maalum ndani ya siku saba, atawasilisha kwa Rais Katiba Inayopendekezwa.

(2) Katibu wa Bunge Maalum atahifadhi nakala mango na tete za Rasimu ya Katiba iliyopitishwa na Bunge Maalum kwa ajili ya kumbukumbu.

(3) Bunge Maalum litaandaa Shughuli maalum ya kitaifa katika tarehe na siku ambayo Mwenyekiti wa Bunge Maalum atakabidhi kwa Rais Katiba Inayopendekezwa.

SEHEMU YA NANE **UTARATIBU WA KUTUNGA MASHARTI YA MPITO NA** **MASHARTI YATOKANAYO**

Utaratibu wa kutunga masharti ya mpito na masharti yatokanayo

90.(1) Mamlaka ya Bunge Maalum ya kutunga masharti ya mpito na masharti yatokanayo yatatekelezwa kwa Bunge Maalum kujadili na kupitisha masharti hayo kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hii.

(2) Mara baada ya Bunge Maalum kukamilisha kazi ya kujadili na kupitisha Katiba Inayopendekezwa, Mwenyekiti wa Kamait ya Masharti ya Mpito na masharti Yatokanayo atawasilisha hoja ya kutunga masharti ya mpito na masharti yatokanayo kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa na Bunge Maalum kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Kanuni ya 75 hadi 78 ya Kanuni hizi.

(3) Kwa madhumuni ya Kanuni hii, “masharti ya mpito” na “masharti yatokanayo” maana yake ni masharti yaliyowekwa katika Sura ya Kaumi na Saba ya Rasimu ya Katiba.

(4) Baada ya masharti ya mpito na masharti yatokanayo kujadiliwa na kupitishwa na Bunge Maalum, Katibu wa Bunge Maalum atawasilisha nakala ya masharti hayo, kama yalivyopitishwa na Bunge Maalum, kwa Rais ili Rais atoe kibali chake kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 97(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(5) Nakala halisi ya Sheria ya Masharti ya Mpito na Masharti Yatokanayo iliyopata kibali cha Rais kwa mujibu wa fasili ya (4) itahifadhiwa na Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.

SEHEMU YA TISA

AMANI NA UTULIVU BUNGENI

Mamlaka ya
Mwenyekiti
wa Bunge
Maalum
kusimamia
utaratibu

91.(1) Mwenyekiti wa Bunge Maalum atakuwa na mamlaka na wajibu wa kuhakikisha kuwa, utaratibu bora unafuatwa katika Bunge Maalum na uamuzi wa Mwenyekiti kuhusu jambo lolote la utaratibu utakuwa ni wa mwisho.

(2) Mjumbe yeyote wa Bunge Maalum atakayekiuka utaratibu uliowekwa na Kanuni hizi anaweza papo hapo kutakiwa na Mwenyekiti afuate utaratibu, na vilevile Mjumbe mwingine yeyote anaweza kusimamia na kumfahamisha Mwenyekiti wa Bunge Maalum kuhusu ukiukwaji wa utaratibu na katika kufanya hivyo, atalazimika kutaja Kanuni ya Bunge Maalum iliyoweka utaratibu uliokiukwa.

Adhabu
zinazoweza
kutolewa na
Mwenyekiti
kwa
ukiukwaji
wa Kanuni

92.(1) Mjumbe yeyote wa Bunge Maalum atakayekiuka Kanuni yoyote ya Kanuni hizi au atakayezungumzia jambo au mambo ambayo hayaruhusiwi na Kanuni hizi, anaweza kuamriwa na Mwenyekiti wa Bunge Maalum ajirekebishe mara moja na kama atakaidi Mwenyekiti atamwamuru akatishe maelezo yake na kukaa mahali pake.

(2) Bila ya kujali masharti ya fasili ya (1), Mwenyekiti wa Bunge Maalum anaweza kumpa onyo Mjumbe yeyote aliyefanya kosa la kukiuka utaratibu uliowekwa na Kanuni hizi, au kosa la kuvuruga majadiliano kwenye Bunge Maalum au uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge Maalum.

(3) Endapo Mjumbe yeyote atatumia maneno au lugha isiyotakiwa Bungeni, yaani lugha ya matusi, usafihi, uchokozi au lugha ya maudhi, na akitakiwa na Mwenyekiti wa Bunge Maalum kujirekebisha kwa kufuta maneno au lugha hiyo akikataa kufanya hivyo, Mwenyekiti anaweza kumwamuru Mjumbe huyo atoke mara moja nje ya Ukumbi wa mikutano ya Bunge Maalum na abaki huko nje kwa muda wote uliosalia wa kikao cha siku hiyo.

(4) Endapo Mjumbe yeyote aliyeamriwa na Mwenyekiti wa Bunge Maalum kutoka nje ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum atakaidi amri hiyo, Mwenyekiti atamwamuru Mpambe wa Bunge Maalum na askari waliopo wamtoe Mjumbe huyo nje ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum na kutokana na kukaidi amri ya Mwenyekiti hatahudhuria vikao vitatu vya Bunge Maalum vinavyofuata.

Adhabu
zinazoweza
kutolewa na
Bunge kwa
ukiukaji wa
Kanuni

93.(1) Mwenyekiti wa Bunge Maalum anaweza kutaja jina la Mjumbe yeyote kwamba amedharau Mamlaka ya Mwenyekiti na kupeleka jina hilo kwenye Kamati ya Kanuni na Haki za Bunge Maalum ikiwa:-

- (a) kwa maneno au vitendo, Mjumbe huyo anaonesha dharau kwa mamlaka ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum;
- (b) Mjumbe huyo kwa makusudi atafanya kitendo chochote cha kudharau Shughuli za Bunge Maalum au kuvuruga mwenendo wa Shughuli za Bunge Maalum.

(2) Kamati ya Kanuni na Haki za Bunge Maalum itajadili suala hilo, na ikithibitika kuwa Mjumbe husika ametenda kosa, inaweza kushauri kwamba:

- (a) ikiwa ni kosa lake la kwanza, Mjumbe huyo asihudhurie vikao vya Bunge Maalum visivyoziidi vitatu; au
- (b) ikiwa ni kosa lake la pili au zaidi, Mjumbe huyo asihudhurie vikao vya Bunge Maalum visivyoziidi vitano.

(4) Bunge linaweza kuzingatia ushauri mwingine wowote utakaotolewa na Kamati ya Kanuni na Haki za Bunge Maalum kuhusu adhabu anayostahili kupewa Mjumbe aliyetenda kosa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hii.

(5) Bila ya kujali masharti ya fasili ya (4), Bunge Maalum linaweza kumchukulia hatua nyingine za kinidhamu Mjumbe yeyote aliyetenda kosa chini ya Kanuni hii, kwa mujibu wa mapendekezo ya Kamati ya Kanuni na Haki za Bunge Maalum.

(6) Adhabu yoyote itakayotolewa kwa Mjumbe aliyekiuka masharti ya Kanuni hii itatolewa kupitia Azimio la Bunge Maalum ambalo litataja adhabu hiyo pamoja na sababu zake.

(7) Mjumbe aliyeadhibiwa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hii, atatoka mara moja katika Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum, baada ya adhabu yake kutolewa.

Mamlaka
maalum ya
Mwenyekiti
ya
kuhakikisha
amani na
utulivu
Bungeni

94. Endapo Mjumbe yeyote wa Bunge Maalum atavunja au atajaribu kuvunja utaratibu au amani na utulivu kwenye Bunge Maalum au ataonyesha tabia za vurugu kwa kutumia nguvu na mabavu ndani ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum, Mwenyekiti wa Bunge Maalum ataamuru Mpambe wa Bunge Maalum amtoe mara moja Mjumbe huyo nje na asihudhurie vikao vya Bunge Maalum na Kamati zake kwa muda wa siku kumi.

Masharti
kwa Mjumbe
aliyesimami-
shwa kazi

95. Mjumbe wa Bunge Maalum aliyesimamishwa kuhudhuria vikao atatoka katika Bunge na hataingia tena katika sehemu yoyote ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum na maeneo ya Bunge na pia hatahudhuria vikao vyovyote vya Kamati za Bunge kwa muda wote atakapokuwa amesimamishwa, na hatalipwa posho nyingine yoyote isipokuwa posho ya kujikimu.

Mamlaka ya
msamaha ya
Mwenyekiti

96. Bila ya kujali masharti yaliyowekwa na Sehemu hii, endapo Mjumbe aliyeadhibiwa ataomba radhi kwa makosa aliyoyafanya, Mwenyekiti anaweza kumsamehe baada ya kuzingatia maoni ya Wajumbe kupitia Kamati ya Kanuni na Haki za Bunge.

Udhibiti wa
fujo Bungeni

97.(1) Kwa madhumuni ya kudhibiti fujo endapo itatokea ndani ya Ukumbi wa Bunge Maalum na iwapo Mwenyekiti wa Bunge Maalum ataona kuwa kuna haja ya kutumia nguvu, basi anaweza kuahirisha Shughuli za Bunge Maalum bila ya hoja yoyote kutolewa, au anaweza kusitisha kikao kwa muda atakaoutaja, ili fujo hiyo iweze kudhibitiwa na Mpambe wa Bunge Maalum.

(2) Baada ya utulivu kurudia, Mwenyekiti wa Bunge Maalum atalipeleka kwenye Kamati ya Kanuni na Haki za Bunge Maalum suala ambalo lilisababisha kutokea kwa fujo ikiwa ni pamoja na jina la Mjumbe au majina ya Wajumbe waliohusika na fujo hiyo ili Kamati hiyo iweze kuzingatia suala hilo na kulishauri Bunge Maalum hatua za kuchukua.

Wajibu wa
Mjumbe
kutunza
amani na
utulivu
Bungeni

98.(1) Kutunza amani na utulivu ndani na nje ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum utakuwa ni wajibu wa kila Mjumbe wa Bunge Maalum.

(2) Bila kujali masharti mengine yaliyowekwa na Sehemu hii, Mjumbe yeyote wa Bunge Maalum atakayefanya kosa la kutotekeleza wajibu wake wa kutunza amani na utulivu kwenye Bunge Maalum, anaweza kuadhibiwa na Mwenyekiti wa Bunge Maalum au na Bunge Maalum.

SEHEMU YA KUMI WAGENI

Ruhusa ya
wageni
Bungeni

99.(1) Wageni wanaweza kuruhusiwa kuingia kwenye Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum katika sehemu yoyote ya Ukumbi huo ambayo itatengwa kwa ajili hiyo.

(2) Wageni wakiwa ndani ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum watalazimika kufuata na kuzingatia masharti yafuatayo:-

(a) watakaa kimya na kwa heshima inayostahili hadi watakapotoka nje ya Ukumbi huo;

- (b) wanapaswa wawe wamevaa mavazi ya heshima;
- (c) wataingia na kutoka Ukumbini kwa staha;
- (d) wasisome kitabu chochote, gazeti, barua au hati nyingineyo ambayo haihusiani na Orodha ya Shughuli za Bunge;
- (e) wasiandike wala kurekodi jambo lolote linalozungumzwa, isipokuwa tu kama ni wawakilishi wa vyombo vya habari;
- (f) inapolazimu kuzungumza, wasizungumze kwa sauti ya juu;
- (g) wasivute sigara au kiko wakati wowote wakiwa ndani ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum au mahali popote nje ya Ukumbi huo ambapo kuna sehemu ya kukaa wageni;
- (h) wazime simu zao za mkononi na kutozitumia kwa namna yoyote wakati wote;
- (i) wasiingie na kamera wala kupiga picha;
- (j) wasishangilie wala kuzomea wakiwa ndani ya Ukumbi wa Bunge Maalum; na
- (k) wasifanye jambo au kitendo chochote ambacho kinaweza kuvuruga amani na utulivu ndani ya Bunge Maalum.

(3) Mwenyekiti wa Bunge Maalum anaweza kumwamuru mgeni yeyote atoke nje ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum endapo atavunja sharti lolote kati ya masharti yaliyotajwa katika fasili ya (2) ya Kanuni hii.

Ruhusa kwa
Waandishi
wa Habari

100.(1) Katibu wa Bunge Maalum anaweza kutoa ruhusa maalumu au ya jumla kwa mwakilishi wa chombo chochote cha habari kuhudhuria vikao vya Bunge Maalum.

(2) Ruhusa yoyote itakayotolewa na Katibu wa Bunge Maalum inaweza kuwekewa masharti yafuatayo:

- (a) chombo husika kitoe maombi rasmi; na
- (b) chombo husika kiteue Waandishi wenye sifa na maadili ya kuweza kuandika habari za Bunge Maalum.

(3) Katibu anaweza wakati wowote kuondoa ruhusa aliyotoa kwa mwakilishi wa chombo chochote cha habari, iwapo chombo hicho kitatoa taarifa yoyote kuhusu Shughuli za Bunge ambayo, kwa maoni ya Bunge, inapotosha ukweli au vinginevyo inakiuka Kanuni, taratibu au haki za Bunge Maalum.

Mamlaka ya
kuwaondoa
wageni
Bungeni

101.(1) Mwenyekiti wa Bunge Maalum anaweza kuamuru wageni watoke nje ya sehemu yoyote ya Ukumbi wa mikutano ya Bunge Maalum na maeneo yake, na anaweza pia kuamuru milango ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum ifungwe.

(2) Endapo wakati wa kikao chochote cha Bunge Maalum Mjumbe wa Bunge Maalum atatoa hoja kuwa wageni watoke nje, Mwenyekiti wa Bunge Maalum atalihoji Bunge papo hapo na hoja itaamuliwa bila ya mjadala au mabadiliko yoyote, wakati wowote atakapoona inafaa kufanya hivyo.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

USALAMA WA MAENEO YA BUNGE MAALUM

Utaratibu wa
kuingia
maeneo ya
Bunge

102.(1) Mwenyekiti wa Bunge Maalum ataweka utaratibu wa kutoa vitambulisho kwa Wajumbe wa Bunge Maalum, watumishi wa Bunge Maalum, watumishi wa Serikali na kwa mtu mwingine yeyote anayeingia kwenye Ukumbi wa Mikutano au maeneo mengine ya Bunge Maalum.

(2) Katibu wa Bunge Maalum atatoa vitambulisho vya aina tofauti kwa ajili ya Wajumbe wa Bunge Maalum, watumishi wa Bunge Maalum, watumishi wa Serikali na wageni wanaokaribishwa katika Ukumbi wa Mikutano na maeneo mengine ya Bunge Maalum.

Ukaguzi

103.(1) Kutakuwa na utaratibu wa kumkagua mtu yeyote anayeingia katika maeneo ya Bunge Maalum kwa kuzingatia:

(a) staha na heshima; na

(b) tofauti ya jinsia.

(2) Mtu yeyote anayeingia maeneo ya Bunge atalazimika kuacha kwenye eneo la ukaguzi simu yake ya mkononi, vifaa vyote vya kielektroniki na vifaa vingine vyovyote ambavyo kwa asili yake vina uwezo wa kurekodi na kuchukua picha.

(3) Endapo katika kufanya ukaguzi mtu yeyote atapatikana na kifaa ambacho kwa asili yake ni cha hatari, mtu huyo atakiacha kifaa hicho kwa walinzi waliopo mlangoni.

(4) Mjumbe, mtumishi au mgeni yeyote atakeyekataa kukaguliwa au kukabidhi kitu chochote ambacho walinzi wataona kwamba kinazuiliwa, hataruhusiwa kuingia ndani ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge au maeneo ya Bunge.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
MENGINEYO

Lugha Rasmi
Bungeni

104.(1) Shughuli za Bunge zitaendeshwa katika lugha ya Kiswahili.

Stahili za
Wajumbe na
Watumishi
wa Bunge
Maalum

105.(1) Kila mtu aliyeteuliwa kuwa Mjumbe wa Bunge Maalum atalipwa posho na malipo mengine kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 29(2) cha Sheria.

(2) Katibu na Watendaji wa Bunge Maalum watalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu kwa namna ambayo Rais ataamua.

Taarifa
Rasmi za
Bunge

106.(1) Taarifa Rasmi ya Majadiliano Bungeni, ikiwa katika lugha iliyotumiwa na msemaji, yakiwa ni maneno halisi aliyotamka, itatayarishwa chini ya usimamizi wa Katibu kwa kufuata maagizo yatakayotolewa na Mwenyekiti kwa ajili hiyo.

(2) Kila Mjumbe aliyetoa hotuba Bungeni atapewa nakala ya hotuba yake mapema iwezekanavyo, ili aweze kusahihisha makosa ya uchapaji, kama yatakuwepo, lakini hataruhusiwa kubadilisha maana halisi ya maneno aliyoyasema Bungeni.

(3) Mjumbe yeyote atakayefanya masahihisho kwa mujibu wa fasili ya (2) atarejesha masahihisho hayo kwa Katibu ndani ya kipindi cha saa ishirini na nne.

Mavazi
Rasmi

107.(1) Mjumbe anayeingia kwenye Ukumbi wa mikutano ya Bunge au ukumbi mwingine wowote ambao kikao cha Kamati ya Bunge kinafanyika, atawajibika kuvaa mavazi nadhifu na yenye kuhifadhi heshima yake, hadhi ya Bunge na utamaduni wa nchi, na yasiwe na alama au rangi inayoashiria Chama chochote cha Siasa.

(2) Vazi Rasmi kwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge litakuwa ni joho lenye kuonesha rangi za Bendera ya Taifa na Nembo ya Taifa lililoshonwa maalumu kwa ajili hiyo, ambalo litavaliwa juu ya vazi lake.

(3) Vazi rasmi la Katibu na Naibu Katibu wa Bunge Maalum na Makatibu Wasaidizi wakiwa ndani ya Ukumbi wa Bunge Maalum litakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Kwa Makatibu wanaume

(i) suti kamili ya kiafrika au suti ya safari, yenye ukosi au shingo ya mviringo na mikono mirefu au mifupi ya rangi nyeusi au bluu na joho maalum la Makatibu Mezani.

(ii) suti kamili ya kimagharibi ya rangi nyeusi au bluu na shati jeupe na tai na joho maalum la Makatibu Mezani.

(b) Kwa Makatibu wanawake

suti ya rangi nyeusi au ya bluu na shati jeupe na tai na joho maalum la Makatibu Mezani.

(4) Mpambe wa Bunge na Wasaidizi wake ndani ya Ukumbi wa Mikutano wa Bunge watavaa mavazi rasmi ambayo yataamuliwa na Mwenyekiti.

(5) Mwenyekiti anaweza kwa sababu maalum, kumruhusu mtu yeyote anayehusika na Shughuli za Bunge kuvaa vazi ambalo sio rasmi.

(6) Mjumbe yeyote wa Bunge Maalum anaweza kutoa taarifa kwenye Bunge Maalum au kwenye Kamati ya Bunge Maalum iwapo Mjumbe mwingine wa Bunge Maalum ataingia kwenye Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum au Ukumbi wa Kamati ya Bunge Maalum akiwa amevaa vazi linalovunja au kukiuka masharti ya Kanuni hii.

(7) Mwenyekiti wa Bunge Maalum au Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Maalum atakaporidhika kuwa Mjumbe wa Bunge Maalum aliyetolewa taarifa kwa mujibu wa fasili ya (6) ya Kanuni hii hajavaa vazi rasmi, ataamuru Mjumbe huyo atoke nje ya Ukumbi wa Bunge au Ukumbi wa Kamati.

(8) Mjumbe wa Bunge Maalum aliyetolewa nje kwa mujibu wa fasili ya (7) ya Kanuni hii, hataingia ndani ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum au Ukumbi wa Kamati ya Bunge Maalum hadi pale atakapokuwa amevaa vazi rasmi.

Ufafanuzi
kutoka Tume
ya
Mabadiliko
ya Katiba

108.(1) Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 20(4) cha Sheria, Bunge Maalum na Kamati yoyote ya Bunge Maalum inaweza kuomba kupata maelezo ya ufafanuzi kutoka Tume ya Mabadiliko ya Katiba kuhusu jambo lolote katika utekelezaji wa majukumu na mamlaka ya Bunge Maalum.

(2) Ufafanuzi kwa mujibu wa fasili ya (1) unaweza kutolewa na Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba au Mjumbe yeyote wa Tume.

Utaratibu
baada ya kifo
cha Mjumbe

109. Endapo Mjumbe atafariki wakati Bunge likiwa katika shughuli zake, Mwenyekiti ataahirisha Shughuli za Bunge kwa siku hiyo kwa ajili ya maombolezo.

Maoni na
ushauri wa
kisheria
kuhusu
Kanuni za
Bunge
Maalum

110.(1) Endapo jambo lolote linalohusu Kanuni za Bunge Maalum litahitaji ushauri wa kisheria, Katibu atalipeleka jambo hilo kwa Mshauri wa Sheria katika Sekretarieti ya Bunge Maalum ili alitolee maoni na ushauri wa kisheria.

(2) Bila kujali masharti yaliyotangulia ya Kanuni hii, maoni na ushauri wa kisheria kuhusu masuala ya kikatiba na kanuni zake unaweza kuombwa kwa wataalam wengine wa sheria kutoka nje ya Bunge Maalum, kama ambavyo Mwenyekiti wa Bunge Maalum, baada ya kushauriana na Katibu wa Bunge Maalum ataona inafaa.

Kutengua
Kanuni

111.(1) Kwa idhini ya Mwenyekiti, Kanuni yoyote inaweza kutenguliwa kwa madhumuni mahsusi baada ya Mjumbe yeyote kutoa hoja kwa ajili hiyo.

(2) Maelezo ya hoja ya kutaka kutengua Kanuni yoyote itakuwa ni pamoja na maelezo kuhusu madhumuni ya kutaka Kanuni hiyo itenguliwe.

(3) Kanuni hiyo itatenguliwa kwa madhumuni yaliyokusudiwa tu na siyo kwa madhumuni mengine yoyote.

Matumizi ya
Ukumbi wa
Mikutano ya
Bunge
Maalum

112 Ukumbi wa Mikutano ya Bunge Maalum hautatumika kwa shughuli nyingine yoyote, isipokuwa kwa shughuli ya uendeshaji wa Mikutano na vikao vya Bunge Maalum na Kamati zake, na pia shughuli nyingine za Bunge Maalum.

Kufanya
mabadiliko
au
marekebisho
katika
Kanuni

113.(1) Bunge Maalum linaweza kuzifanyia mabadiliko au marekebisho Kanuni hizi kwa Azimio litakalowasilishwa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Haki za Bunge.

(2) Endapo Mjumbe yoyote wa Bunge Maalum ataona kuna haja ya Kanuni fulani kufanyiwa mabadiliko au marekebisho, anaweza kuwasilisha mapendekezo yake pamoja na sababu zake, kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Haki za Bunge ili yafanyiwe kazi na Kamati hiyo, na kama yataonekana yanafaa, yatawasilishwa Bungeni kwa mujibu wa fasili ya (1).

NYONGEZA YA KWANZA

KANUNI ZA UCHAGUZI WA MWENYEKITI NA MAKAMU MWENYEKITI [Chini ya Kanuni ya 11(4)]

SEHEMU YA KWANZA UTANGULIZI

- Jina 1. Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum, 2014.
- Matumizi 2. Kanuni hizi zitatumika katika mchakato wa Uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum.
- Tafsiri 3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa pale ambapo maelezo yatahitajika vinginevyo-
- “Mgombea”** ni Mjumbe wa Bunge Maalum aliyejitokeza au aliyependekezwa na Mjumbe mwingine au Wajumbe wengine wa Bunge Maalum kuwa mgombea wa Uchaguzi wa nafasi ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum;
- “Msimamizi wa Uchaguzi”** ni Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Katibu wa Baraza la Wawakilishi ambao kwa mujibu wa Kanuni hizi, wamepewa mamlaka ya kuendesha na kusimamia mchakato wa Uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum;
- “Mwenyekiti”** ni Mjumbe wa Bunge Maalum aliyechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge Maalum kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 23(1) cha Sheria;
- “Mwenyekiti wa muda”** ni Mjumbe wa Bunge Maalum aliyechaguliwa kwa mujibu wa kifungu cha 22A cha Sheria awe Mwenyekiti kwa ajili ya kusimamia uchaguzi wa Mwenyekiti wa Bunge Maalum;
- “Nafasi”** ni nafasi iliyo wazi ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum;
- “Nafasi ya nasibu”** ni nafasi iliyo wazi ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum isiyotokana na kuundwa upya kwa Bunge Maalum;
- “Siku ya uteuzi”** ni siku ambayo imetangazwa na msimamizi wa uchaguzi kwamba ni siku ya mwisho ya kupokea majina ya wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum;
- “Uchaguzi”** ni Uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum.

SEHEMU YA PILI
USIMAMIZI WA UCHAGUZI NA UWASILISHAJI WA JINA LA MGOMBEA

Uendeshaji
na
usimamizi
wa uchaguzi
wa
Mwenyekiti
na Makamu
Mwenyekiti
wa Bunge
Maalum

4. Uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum utaendeshwa na kusimamiwa na Mwenyekiti wa muda wa Bunge Maalum, kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Kanuni za Bunge Maalum, pamoja na Kanuni hizi.

Kuwasilisha
jina la
mgombea

5.(1) Mara baada ya kukalia kiti, Mwenyekiti wa muda atawaalika Wajumbe wa Bunge Maalum wenye sifa ya kuwa wagombea wa uchaguzi wa nafasi ya Mwenyekiti wa Bunge Maalum na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum kuwasilisha majina yao kwa Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Katibu wa Baraza la Wawakilishi.

(2) Kila jina la mgombea wa uchaguzi wa nafasi ya Mwenyekiti wa Bunge Maalum, atatakiwa kujaza fomu iliyoandaliwa kwa ajili hiyo ambayoi itakuwa na majina ya Wajumbe ishirini wa Bunge Maalum wanaounga mkono mgombea husika, kwa idadi ya Wajumbe kumi kwa kila upande wa Jamhuri ya Muungano.

(3) Fomu za Wagombea wa uchaguzi wa nafasi ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum kwa mujibu wa masharti ya fasili ya (2) zitawasilishwa kwa Msimamizi wa Uchaguzi, ofisini kwake, kabla ya saa nne asubuhi ya siku ya uteuzi.

(4) Baada ya kupokea majina ya wagombea kwa mujibu wa masharti ya fasili ya (3), Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Katibu wa Baraza la Wawakilishi **wataandaa** karatasi za kura zinazoonyesha majina na wagombea wote wa uchaguzi wa nafasi ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum, waliotimiza masharti yaliyowekwa na Kanuni za Bunge Maalum, pamoja na masharti ya Kanuni hizi, na wakati wa kupiga kura, atatoa karatasi moja tu ya kura kwa kila Mjumbe wa Bunge Maalum.

SEHEMU YA TATU
UPIGAJI WA KURA

Kujitoa
katika
uchaguzi

6. Muda mfupi kabla ya uchaguzi, mgombea yeyote anaweza kutoa taarifa ya maandishi kwa Msimamizi wa Uchaguzi kuwa anajitoa kugombea, na Msimamizi wa Uchaguzi atawasilisha jina hilo kwa Mwenyekiti wa muda ambaye atatangaza jina hilo kwamba limefutwa kutokana na sababu ya kwamba mgombea ametoa taarifa ya kujitoa katika uchaguzi huo.

Upigaji wa
kura

7.(1) Kila mjumbe atatakiwa kupiga kura ya siri kwa kuweka alama ya vyema “(√)” kwenye kisanduku kilichopo pembeni mwa jina la mgombea anayemtaka awe Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum na kutumbukiza karatsi hiyo katika sanduku maalum la kura lililoandaliwa kwa ajili hiyo.

(2) Baada ya kuridhika kwamba Wajumbe wote wamepiga kura na kutumbukiza karatasi zao za kupigia kura kwenye masanduku ya kura, Katibu atayakusanya masanduku yote na kuyapeleka kwenye chumba maalum cha kuhesabia kura, na kura zitahesabiwa mbele ya Wawakilishi walioteuliwa na wagombea, mmoja kwa kila mgombea.

(3) Mgombea yeyote atakuwa amechaguliwa kuwa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum kama atapata zaidi ya nusu ya kura za Wajumbe wote, na iwapo hakutakuwa na mgombea aliyepata zaidi ya nusu ya kura hizo, uchaguzi utarudiwa:

Isipokuwa kwamba, ni wagombea wawili tu watakaokuwa wamepata kura nyingi zaidi ndio watakaopigiwa kura, na katika hatua hiyo, mgombea atakayepata kura nyingi zaidi atatangazwa kuwa ndiye mshindi.

(4) Endapo wagombea wawili au zaidi watapata kura sawa, basi wagombea hao tu ndio watakaopigiwa kura, na mgombea atakayepata kura nyingi zaidi atatangazwa kuwa ndiye mshindi.

(5) Iwapo wagombea wawili au zaidi watapata kura sawa katika nafasi ya pili na yule wa kwanza hakupata zaidi ya nusu ya kura zilizopigwa, basi wagombea hao wawili pamoja na yule wa kwanza ndio watakaopigiwa kura, na mgombea atakayepata kura nyingi zaidi atatangazwa kuwa ndiye mshindi.

(6) Endapo awamu ya pili ya upigaji wa kura itashindwa kumpata mshindi, basi Mwenyekiti wa muda atapiga kura yake ya uamuzi ili mshindi apatikane.

(7) Endapo kutakuwa na mgombea mmoja tu, basi mgombea huyo atapigiwa kura ya “Ndiyo” au “Hapana”, na atatangazwa kuwa amechaguliwa kuwa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum iwapo atapata kura za “Ndiyo” za idadi ya zaidi ya nusu ya kura za Wajumbe wote.

SEHEMU YA NNE
KUTANGAZA MATOKEO YA UCHAGUZI NA KUAPISHWA
KUSHIKA MADARAKA

Kutangaza
matokeo ya
uchaguzi
Sura 83

8. Mara baada ya mshindi kupatikana, Msimamzi wa Uchaguzi atamtangaza Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum aliyechaguliwa, na Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti huyo Mteule ataapa

viapo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Bunge Maalum.

Mwenyekiti/
Makamu
Mwenyekiti
kula yaamini
/kiapo

9.(1) Muda wa Mwenyekiti wa Bunge Maalum Mteule kuapishwa utakapowadia, Mwenyekiti wa muda atamwita Mwenyekiti wa Bunge Maalum Mteule apite mbele ya Bunge Maalum ili ale yamini au aape viapo vinavyomhusu.

Sura 83

(2) Mjumbe yeyote wa Bunge Maalum aliyechaguliwa kuwa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum, kabla ya kushika madaraka yake ataapa mbele ya Bunge Maalum **Kiapo cha Utii na Kiapo cha Mwenyekiti** au **Makamu Mwenyekiti** vilivyowekwa na Sheria na Kanuni za Bunge Maalum.

(3) Bila ya kuathiri masharti yoyote ya Kanuni hizi, Uchaguzi wa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum utaendeshwa kwa utaratibu ule ule unaotumika kumchagua Mwenyekiti wa Bunge Maalum.

FOMU YA KUPENDEKEZA JINA LA MGOMBEA
[Chini ya Kanuni ya 5(2)]

KUPENDEKEZA MGOMBEA

[Ijazwe na Mjumbe anayependekeza]

Kwa Msimamizi wa Uchaguzi wa Mwenyekiti/Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum.

Mimi..... nikiwa Mjumbe wa Bunge Maalum,

nampendekeza ambaye ni Mjumbe wa Bunge Maalum kuwa mgombea wa uchaguzi wa nafasi ya Mwenyekiti/Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum.

Taarifa muhimu kuhusu mgombea ninayempendekeza ni kama ifuatavyo:-

1. Jina Kamili la Mgomba:.....
2. Umri wake:
3. Jinsia:
4. Kiwango cha Elimu:.....
5. Anuani yake:

Jina la Mjumbe anayependekeza:

Saini yake:

Pendekezo hili linaungwa mkono na Wajumbe wafuatao:-

A: Wajumbe Kumi kutoka Tanzania Bara

Jina

Saini

.....
.....
.....

.....
.....
.....

.....	
.....	
.....	
.....	
.....	
.....	
.....	

B: Wajumbe Kumi kutoka Tanzania Zanzibar

Jina

Saini

.....	
.....	
.....	
.....	
.....	
.....	
.....	
.....	
.....	
.....	

